**POLEPOLE** afunga mjadala muda JPM kuendelea kuwa madarakani



UKURASA 3

**AWACHOMA** visu watoto tumboni mkewe kuolewa

UKURASA 5



**Zidane: Siwezi kuitenga Madrid**

UKURASA 21


# Nipashe

Jumatano Februari 10, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580487

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710


# Nape acharukia ukusanyaji kodi

UKURASA 2





Mbunge wa Mtama, Nape Nnauye

**MAHOJIANO MAALUM:**

## Dk. Mwinyi asema yeye si muumini kodi kubwa

**ATAJA** mambo 10 siku 100...

*Endelea Uk. 3 & 4*

## YALIYOMO

UKURASA WA 7

### AMRI YA SERIKALI YAWAPELEKA SHULE WATOTO WA MCHUNGAJI

HATIMAYE watoto waliozuiwa kwenda shule na baba yao ambaye ni mchungaji, wameanza masomo katika Shule ya Msingi Buyekera iliyopo Manispaa ya Bukoba mkoani Kagera, kwa amri ...

### SPIKA AWAPIGA 'KOMBORA' WASOMI

UKURASA 2

UKURASA WA 7

### MPANGO WAIVA SEKTA NDOGO YA FEDHA

OFISI ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) imefanya uteuzi wa watu 212 katika ngazi za wizara, mikoa na halmashauri kwa ajili ya uratibu...

**MICHEZO** SIMBA NA MAJEMBE 27 WAIFUATA VITA KWA VITA UK. 24

MAONI, KATUNI UK. 6

# Nape acharuka vikosi kazi ukusanyaji kodi

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

MBUNGE wa Mtama (CCM), Nape Nnauye, amesema ukusanyaji kodi kupitia vikosi kazi unaua biashara, hivyo kushauri kazi hiyo ifanywe na wenye taaluma chini ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Nape alisema hayo jana wakati wa mjadala wa mapendekezo ya mwongozo wa maandalizi ya mpango, bajeti ya serikali na mpango wa maendeleo wa taifa kwa mwaka 2021/22 na mapendekezo ya mpango wa tatu wa maendeleo wa taifa wa miaka mitano wa mwaka 2021/22 -2025/26.

"Ushauri wangu kwa serikali, hebu punguzeni habari ya 'task force' kukusanya kodi, si kazi yao, wao wanakwenda kuua biashara," alisema.

Nape alisema ukusanyaji wa kodi ni taaluma, lakini tatizo lililopo ni kwamba serikali imeamua kuacha kuwatumia wanataaluma ambao ndio wakusanya kodi na kuamua kutumia 'task force' (kikosi kazi) kukusanya kodi.

"Task force kwa sababu si taaluma yao, wanachofanya wanakwenda kuua biashara. Kelele hizi zote unazozisikia ni kwa sababu tumeamua kuacha kutumia taaluma ya ukusanyaji wa kodi. Tumeamua kutumia 'task force' kukusanya kodi na kwa sababu si taaluma yao, wanachoangalia ni kufikia lengo walilowekewa.

"Sasa kinachotokea wanakwenda kwa mfanyabiashara, hawajali maisha yake ya kesho, hawajali kwamba wanatakiwa wakusanye kodi leo, wamwachie uwezo wa kuzalisha ili wakusanye na kesho. Tunafurahia matokeo ya muda mfupi.

"Ni kweli tumefanya kazi nzuri ya kukusanya kodi, lakini hayo matokeo tunayoyafurahia ni ya muda mfupi sana kwa sababu idadi ya biashara zinazofungwa ni nyingi mno," alisema.

Nape alishauri serikali kupunguza habari ya 'task force' kukusanya kodi kwa kuwa si kazi yao na kusisitiza kwamba baadhi ya watu hao wanakwenda mahali tayari na hati ya mashtaka ya kesi za uhujumu uchumi na wanawatisha watu.

"Ushauri wangu serikali ondokeni kwenye task force rudini kwenye taaluma ya ukusanyaji wa kodi, itatupa uhalali wa kuendelea kukusanya kodi kesho na kesho kutwa," alisisitiza Nape.

Naye Mbunge wa Geita Mjini (CCM), Costantine Kanyasu, akisema ni lazima Wizara ya Fedha na Mipango iwasikilize wananchi na inawezekana hawana taarifa sahihi, hivyo biashara zinakufa.

"Tuwapongeze sana TRA (Mamlaka ya Mapato Tanzania) kwa kukusanya pesa nyingi, lakini iko shida. Nimemsikiliza mtu mmoja wa TRA kwenye TV alikuwa anaongea, akasema sawa biashara zinafungwa, lakini zinafunguliwa nyingi zaidi.

"Tumesema kwa miaka mitano kuna tatizo. Hii kitu inaitwa 'task force', tulifanya mkutano na mheshimiwa (Medard) Kalemani (Waziri wa Nishati pale Geita na wafanyabiashara wa mkoa wa Geita. Wanalalamikia TRA makadirio yao si rafiki na kwa nini si rafiki inawezekana ni kwa sababu ya target (malengo ya kukusanya kodi). Target ni kubwa kuliko survey (utafiti) iliyofanyika ya uwezo wa walipa kodi," alisema. "Task force inafanya jambo moja. wanakuja wanafanya special audit (ukaguzi maalum). Wakifanya wanakuambia unatakiwa kulipa Sh. bilioni tano, wakati huyu mteja ana appeal (anakata rufani) wanazuia akaunti wanachukua pesa zote kwenye akaunti.

"Ukikuta kuna pesa kwenye akaunti ya mfanyabiashara leo kwa mfano biashara ya utalii, pesa si zake pesa ni za wateja wanaosubiri huduma. Unapozizuia maana yake unazuia asitoe huduma kwa huyo mtalii. Unazuia asilipe mishahara, unazuia asiendelee kufanya kazi," alisema.

Kutokana na mjadala huo, Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson, alisema jambo hilo limeshafika kwa Waziri Mkuu, hivyo ni vyema wakawa na subira.

# Ndugai awapiga rungu wasomi

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amesema uchumi wa nchi kwa sasa umeshikiliwa na watu wa darasa la saba na kushuka chini kwa kuwa ndio wazalishaji na wafugaji wakuu.

Ndugai alikuwa akikazia hoja iliyotolewa na Mbunge wa Geita Vijijini (CCM), Joseph Musukuma, aliyedai kuwa Watanzania wengi ambao ni darasa la saba, ndio wametoa mchango mkubwa katika kukuza uchumi, huku akiitaka serikali iwaangalie na kuwawezesha.

Musukuma alitaka mpango huo uangalie hali halisi ya uchumi nchini, kwa kuwa hali si nzuri na biashara nyingi zimefungwa kutokana na vikwazo mbalimbali ikiwamo utitiri wa kodi.

Wabunge walikuwa wakijadili, mapendekezo ya mwongozo wa maandalizi ya mpango, bajeti ya serikali na mpango wa maendeleo wa taifa kwa mwaka 2021/22 na mapendekezo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano wa mwaka 2021/22 -2025/26.

Wakati anaeleza darasa la saba na kurudi chini walivyoshika uchumi, Spika Ndugai alisema: "Wasomi wangapi wanalima? Wangapi wanafuga? Na sasa hivi kila mtoto anayefaulu haendi kufuga, wala kulima.

Anayemaliza 'form four' (kidato cha nne) anaona tayari ameondokana na kilimo. Nyie mnasema tulime sijui hekari ngapi za mahindi, nani atakusaidia kuvuna? Kuna form four hata mmoja atakusaidia kuvuna?" Alihoji.

Akionyesha kuchukizwa na hali hiyo, Spika Ndugai alihoji: "Ni kweli jamani. Kwa nini kila mama anataka kila 'house girl' (mfanyakazi wa ndani) atoke Iringa? Kwa nini asije Dodoma kuchukua Wagogo? Ni kwa sababu Iringa wanachapa kazi sana."

Kwa minajili hiyo, Spika Ndugai alisema tatizo hilo linatokana na ukweli kwamba hakuna mfumo wa elimu unaotengeneza vijana kupenda kuzalisha.

"Sijui tufanye nini maana hata mimi sijui, lakini ukweli ni kwamba tunatengeneza vijana wanaopenda kucheza pool (mpira wa meza) na kushika simu na kuchati, ndiyo maana waheshimiwa wabunge kwenye huu mpango ni mahali tunapotakiwa tufikiri tuitoe nchi yetu mahali ilipo. Sisi ndio washauri wakuu wa serikali," alisema.

**WAWAJIBIKAJI WACHACHE**

Spika Ndugai alisema Rais John Magufuli anajitahidi na kufanya kazi sana, lakini kwa bahati mbaya wanaofanya kazi kwa kiwango chake ni wachache sana.

"Huu ndio ukweli tutaweza kuifanya nchi iwe na mpangilio wa utendaji. Kila mtu apewe kazi na apimwe kwa anachokifanya na hasa walioajiriwa serikali ndio kabisa, watumishi, hivi tufanye nini kuhakikisha kila mtu anafanya kazi?

"Kama kweli mabwana shamba wa nchi hii wanafanya kazi inavyopaswa, kama kweli maofisa maendeleo wa jamii wa nchi hii wanafanya kazi na hawapokei mshahara wa bure. Nyie ni wabunge mmewaona maofisa maendeleo ya jamii wanafanya kazi wapi."

"Watanzania hatuna hata ile passion (ari) ya kufanya kazi, utaona hata timu yetu ya taifa ikienda kucheza huko nje, haijitumi wala haifanyi kazi, huoni wakitafuta goli kama wenzao, sasa tuna tatizo gani jamani? Inabidi kuangalia namna ya kuwabadilisha Watanzania tabia zao ili wapende kujituma na kuchangamkia fursa," alisisitiza.

Mbunge wa Mlimba (CCM), Godwin Kunambi, alisema mipango iliyowasilishwa na serikali ni zao la malengo ambalo linatoa mikakati na mbinu ya kutekeleza malengo ya serikali.

Alisema kupitia mpango huo katika eneo la kilimo ni wazi kuwa asilimia 65 ya Watanzania wanapata kipato chao kupitia kilimo ambacho nacho kinachangia asilimia 27 kwenye pato la taifa, ambazo kati ya hizo asilimia 24 ni mauzo ya nje ya nchi.

"Bado tuna kazi kubwa katika kilimo, kilimo chetu tunafanya kwa ajili ya kula kitu ambacho bado kina safari ndefu sana. Nchi kama Tanzania yenye ardhi kubwa. Japan kwa mwaka mzima wananunua chakula kwa mwaka mzima wananunua chakula Afrika, lakini Zimbabwe kwa nini isiwe Tanzania? Alihoji.

"Ifike mahali viongozi wakichaguliwa wapewe miezi sita wapimwe kama wakishindwa kufanya vizuri waondolewe, kuna watu wanawekwa mahali wanashindwa kuleta mabadiliko yeyote hata kubadilisha tu kiti alichokikalia," alisisitiza.

"Sekta ya ardhi bado haijafanya kazi, nchi hii inaweza kupimwa tuna halmashauri 185, lakini hatuwezi hata kupima halmashauri 50, kuna haja ya kuwapo kweli?

Alisema Dodoma kwa miaka mitatu iliyopita ilikuwa haijapimwa. "Mimi nimepima viwanja 2,000 bila serikali kuu, tukipima nchi nzima serikali itapata fedha nyingi, ardhi ikipimwa ni mtaji kwanza tunaongeza wigo wa kodi. Kuna pesa kwenye ardhi, tunaweza kupata fedha za bajeti mara ya mbili ya hizi za bajeti."

Katika hoja hiyo, Spika Ndugai aliongeza baada ya kauli hiyo ya Kunambi akitolea mfano nchi ya Kenya kwamba imepima radhi yake takribani yote ndiyo maana bajeti yao ni mara mbili ya bajeti ya Tanzania.

"Mnaweza msione point yake (Kunambi), lakini ni ukweli halisi, mashamba yote yakipimwa nchi hii ikipimwa, tutapata fedha nyingi sana, hakutakuwa na yale sijui tukate kodi kwenye simu, sijui kwenye mafuta tutapata fedha nyingi," alisema.

Mbunge wa Musoma Vijijini, Prof. Sospeter Muhongo (CCM) alisema kupitia mipango hiyo mizuri serikali haina budi kufanyakazi kwa bidii kuhakikisha nchi haishuki na kurejea kwenye uchumi wa chini baada ya kupanda na kufikia uchumi wa kati wa chini.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAMLAKA YA MAENEO MAALUM YA UZALISHAJI KWA MAUZO YA NJE (EPZA)

TANGAZO KWA WADAIWA WOTE WA MAMLAKA YA EPZ

1. Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje (EPZA) inawatangazia WADAIWA wake wote kufika katika Ofisi za Mamlaka kwa lengo la kulipa malimbikizo na madeni yao yote kama vile kodi ya pango, ada za leseni na tozo mbalimbali NDANI YA MUDA SIKU SABA ZA KAZI kuanzia tarehe ya tangazo hili.

2. WADAIWA wote wanaelekezwa kutumia fursa hii kulipa madeni yao kwa wakati na baada ya muda huu uliowekwa kwenye tangazo kuisha. Mamlaka haitasita kuchukua hatua zote za kisheria zilizopo kukusanya madeni hayo, ikiwemo kusitisha huduma za uwezeshaji, kufungua kesi Mahakamani kwa lengo la kukusanya madeni ambapo gharama pamoja na riba za ucheleweshaji zitaangaliwa na kutumika.

3. Mamlaka inawashukuru wateja wake wote walioweza kulipa madeni na malimbikizo ya madeni yao kwa wakati.

IMETOLEWA NA KAIMU MKURUGENZI MKUU
10/02/2021

Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uwekezaji kwa Mauzo Nje (EPZA)
Mabibo External, Mandela Road, Makao Makuu, S.L.P. 12112,
Dar es salaam, Tel: +255222925058-60 Nukushi: +255222925061,
Barua Pepe: info@epza.go.tz, Tovuti: www.epza.go.tz

HABARI KITAIFA

# Mwinyi ataja mambo 10 siku 100

**Na Romana Mallya**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameeleza maeneo 10 ambayo ameyatekeleza ndani ya siku 100 tangu aingie madarakani, kubwa ni kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa ambayo imeondoa malumbano, chuki na kujenga umoja wa wananchi.

Akizungumza na wahariri na waandishi wa habari jana, Ikulu Zanzibar, kuhusu mafanikio ya serikali ya awamu ya nane ikiwa ni siku 100 tangu kuapishwa kwake, Rais Mwinyi alisema kuundwa kwa serikali hiyo kwake ni moja ya mafanikio makubwa.

Alisema baada ya kuingia madarakani alitambua kuwa hawawezi kufanikiwa kuleta maendeleo kama hakuna mambo ya msingi ambayo ni amani na umoja wa wananchi.

"Ninamshukuru Mungu amani tunayo, ninawashukuru Wazanzibari wote pamoja na vyombo vya ulinzi na usalama kwa kulinda na kuendeleza amani tuliyonayo.

"Niliona kuna umuhimu wa kama kiongozi wa nchi niwaunganishe wananchi tutafute umoja wa kitaifa, ndipo tulipoanza mazungumzo kati yetu na viongozi wa ACT-Wazalendo, ninawashukuru kwa kukubali kufanya mazungumzo na kuwa na Serikali ya Umoja wa Kitaifa."

Rais Mwingi alisema aliona bila serikali ya umoja wa kitaifa, wangepata shida ya kuleta maendeleo kwa sababu mazingira bado yangewasumbua.

"Kuunga kwa serikali ya umoja wa kitaifa kumefanikiwa mambo makuu matatu, kwanza tumekidhi matakwa ya kikatiba, Katiba inataka serikali ya Umoja wa Kitaifa iundwe endapo chama kitakachokuwa cha pili kitapata zaidi ya asilimia 10.

"Tumeleta umoja wa wananchi wetu, yale malumbano na chuki yaliyokuwapo tunaziona kwa kiwango kikubwa zimeanza kupungua na wananchi wanazungumzia maendeleo na tumeacha kulumbana kisiasa. Tumeweka mazingira mazuri ya kisiasa ili kuleta maendeleo ya kiuchumi."

Eneo la pili, ni kuundwa kwa serikali iliyopunguzwa ukubwa na gharama za utawala na fedha nyingi zaidi kuelekezwa kwenye miundombinu na huduma za jamii.

Eneo la tatu alisema ni la uchumi ambapo walijinadi kwa 'sera ya uchumi wa bluu' na alipoingia madarakani alifanya kazi kubwa ya kuzungumza na wawekezaji ili tutengeneza mazingira bora na tayari wameshatia saini ya baadhi yake na hivi karibuni watakamilisha mpango wa kukopa Benki ya Dunia (WB) ili kujenga miundombinu ya umeme.

Eneo la nne ni miundombinu ambapo baada ya kuapishwa alikwenda Bandari ya Malindi na kufanya mabadiliko ya uongozi na hivi karibuni wakifungua terminal mpya ya tatu watakuwa na mwekezaji watakayeingia naye makubaliano ya kuiendesha na kuwekeza zaidi katika mizigo.

"Kwenye mapato bandari ile kwa mwaka mmoja ilikuwa ikiingiza faida Sh. bilioni 4.3, lakini kwa mwezi Desemba peke yake wameingiza faida Sh. bilioni 2.1," alisema.

Rais Mwinyi alisema katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume walifanya mabadiliko ya uongozi na hivi karibuni wakifungua terminal mpya ya tatu watakuwa na mwekezaji watakayeingia naye makubaliano ya kuiendesha na kuwekeza zaidi katika mizigo.

Eneo la tano ni mikutano na wadau wa biashara, afya na elimu ambapo alisema katika sekta ya utalii kila siku amekuwa akikutana na wawekezaji kutoka nje ya nchi.

Eneo la sita alilitaja ni uwajibikaji, na kwamba aliwataka mawaziri na makatibu wakuu kuhakikisha wanausimamia walio chini yao kufanya kazi.

Eneo la saba ni la utawala bora ambapo vita dhidi ya rushwa, ubadhirifu, wizi wa mali za umma wamelivalia njuga na hivi karibuni wamesimamishwa wafanyakazi zaidi ya 80, baada ya kuthibitika wanacheza na mitandao ya mapato na matumizi ya serikali na wengine wana kula rushwa.

Eneo la nane ni la ukusanyaji wa mapato ya kodi na yasiyo ya kodi ambayo mwezi Desemba, 2020 jumla ya Sh. bilioni 101 zilikusanywa sawa na asilimia 109 ya makadirio ya Sh. bilioni 93 ya Desemba kwa mwaka uliopita.

Alisema mapato hayo yameonyesha ongezeko la asilimia 46 yakilinganishwa na Sh. bilioni 55 zilizokusanywa Oktoba mwaka jana.

Eneo la tisa ni la udhalilishaji, ambalo wameimarisha uchunguzi kwa kulitaka Jeshi la Polisi na Wizara ya Afya kuhakikisha vituo vya uchunguzi vinafanya kazi ya ziada na Mkurugenzi wa Mashtaka kuhakikisha kesi zinakwenda mahakamani haraka.

Alisema ameagiza Baraza la Wawakilishi linalotarajia kukaa leo, serikali ipeleke mapendekezo ya kubadilisha sheria ili makosa ya udhalilishaji yasiwe na dhamana.

Alitaja eneo la kumi ni ushirikiano wa sekta binafsi ambapo wadau mbalimbali zikiwamo benki zimeonyesha nia ya kushirikiana, na kwamba serikali itaendelea kuboresha mazingira ya biashara.

## Polepole amaliza mjadala JPM muda urais

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

MBUNGE wa kuteuliwa, Humphrey Polepole, amemaliza mjadala wa wabunge kutaka Rais John Magufuli aongezewe muda wa kukaa madarakani.

Polepole amesema Rais Magufuli hana mpango wa kuongeza muda wa kukaa zaidi madarakani pindi atakapomaliza muhula wa pili wa utawala wake.

Polepole ambaye ni Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC), Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), alitoa kauli hiyo jana, Bungeni, baada ya kuomba kutoa taarifa kwa Mbunge Khatib Said Haji (Konde-ACT Wazalendo), aliyegusia jambo hilo.

Wabunge walikuwa wakijadili mapendekezo ya mwongozo wa maandalizi ya mpango, bajeti ya serikali na mpango wa maendeleo wa taifa kwa mwaka 2021/22 na mapendekezo ya mpango wa tatu wa maendeleo wa taifa wa miaka mitano wa mwaka 2021/22 -2025/26.

Haji, licha ya kumpongeza Rais Magufuli kwa msimamo wake wa kuilinda na kuitetea katiba, hususani kutotaka kuongeza muda wa kusalia madarakani, alisema baadhi ya wabunge wake wanamwomba aongeze muda, akiwa tayari ameweka msimamo wa wazi.

Alisema Rais Magufuli alimtuma Polepole, awaambie wana CCM, Rais hana shida ya kuongeza muda.

Wakati mbunge akiendelea na mchango wake, Polepole alisimama na kumwomba Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, kutoa taarifa.

"Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutumia nafasi hii kumpa taarifa Mheshimiwa Mbunge aliyekuwa akiendelea kusema masuala ya Chama Cha Mapinduzi yanazungumziwa kwenye vikao vya Chama Cha Mapinduzi.

"Hapa Bungeni, wabunge wana uhuru wa kutumia uhuru wa Bunge kuzungumza, lakini kinachozungumzwa humu ndani hakiathiri msimamo wa Chama Cha Mapinduzi ambao tumekwisha utoa.

"Msemaji wa chama ni ndugu John Pombe Joseph Magufuli na kama si yeye, nasema kwa niaba yake kwamba Rais hatoongeza muda. Lakini hii isizuie watu kuzungumza humu Bungeni.

Alipokuwa akichangia mapendekezo hayo, Khatibu alisema: "Kwenye suala la utawala bora, kwanza nampongeza mheshimiwa Rais kwa uamuzi wake wa kuiheshimu katiba ya nchi hii. Kabla yote alitangulia kuapa kulinda na kuitetea.

"Mheshimiwa Rais ameendelea kuwa mlinzi wa katiba, kwa uamuzi wake wa kumtuma Humphrey Polepole, awaambie wana CCM kwamba hatoongeza kipindi cha utawala, ni ishara ya Rais wetu kuilinda na kuienzi katiba.

"Atakuwa Rais wa kwanza katika ukanda wa nchi za Afrika, ambaye baadhi ya wabunge wake wanamuomba aongeze muda, lakini tayari ameweka msimamo wa wazi na alimtuma Polepole, awaambie CCM, Rais hana shida ya kuongeza muda.

"Alikutuma (Polepole) na video zinatembea tunaziona. Kwanini unawaacha wakina Sanga (Deo Sanga) hapa wanaendelea kupotosha? Kwanini hamuheshimu mawazo ya mheshimiwa Rais?"

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI KISUTU
DAR ES SALAAM

SHAURI LA MADAI No. 189 YA MWAKA 2020

M.M.INDUSTRIES........................................................................ MDAI

DHIDI YA

GEAT LAKES CONSTRUCTION COMPANY LTD...............................MDAIWA

KWA
THE MANAGING DIRECTOR,
GREAT LAKES CONSTRUCTION CO LTD,
BOX 135,
DAR ES SALAAM

KUITWA SHAURINI

Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala ya madai ambayo inaweza kupatikana katika Mahakama hii,unahitajika kuhudhuria katika Mahakama hii binafsi ,Wakili wako au mwakilishi ambaye anaruhusiwa kisheria, siku ya tarehe **24/02/2021 saa 7.00** Mchana.

**ANGALIA:**
Kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama ikithibitisha kuwa umepokea wito huu wa kuitwa shaurini na hukufika itaendelea na kutoa kutoa maamuzi bila wewe kuwepo

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe **21** Mwezi wa **01** Mwaka **2021**

HAKIMU MKAZI MWANDAMIZI
KISUTU -DAR ES SALAAM

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
KISUTU - DAR ES SALAAM

HABARI KITAIFA

## MAHOJIANO MAALUM -2

# Rais Mwinyi: Mimi si muumini kodi kubwa

- Asisitiza 'kutofukua makaburi'
- Aagiza wizara kupitia kodi zote
- Ufisadi serikalini, sekta binafsi...




**Na Sanula Athanas**, ZANZIBAR

KATIKA sehemu ya kwanza jana, Rais Hussein Ali Mwinyi, alifafanua mwelekeo wa utendaji wa kiserikali anayoiongoza, akianika mikakati ya kuhakikisha wanatoa ajira nyingi kwa wananchi.

Dk. Mwinyi pia alibainisha namna maridhiano visiwani Zanzibar, yanavyowapa mwanga wa kuiletea maendeleo, akipongeza mafanikio yaliyopatikana kutokana na Chama cha ACT-Wazalendo kukubali kuungana naye kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Endelea kufuatilia mazungumzo ya Nipashe na kiongozi huyo:

**SWALI: Kipo kilio cha biashara kufungwa kutokana na kodi. Serikali yako ina mkakati gani katika hili?**

**RAIS MWINYI:** Mimi si muumini wa kodi kubwa. Ninaamini kwamba kodi ndogo ndizo zinazoleta mapato makubwa zaidi kwa sababu watu wakimudu kulipa, watalipa wengi. Kwa hiyo, tutakuwa na wafanyabiashara wengi na tutapata kodi kubwa zaidi.

Ukizipandisha utapata wachache na mwisho wa siku utakachokikusanya ni kidogo sana. Kwa hiyo, ninawataka (wafanyabiashara) zile kodi ndogo zitakazowekwa, asiwapo tena mtu wa kukwepa. Sote tuhakikishe tunazilipa.

Kwa hiyo, nimetoa maelekezo kwamba kodi zetu zote tuzitazame upya ili pale ambapo pana uwezekano wa kuzishusha, tuzishushe. Lakini, baada ya kufanya hivyo, tuhakikishe kila mtu anawajibika kulipa kodi.

Kuna kodi ambazo kuzikusanya ni gharama zaidi kuliko kuziacha zisiwapo. Kwa hiyo, nikatoa maelekezo kwa wenzetu wa Wizara ya Fedha kuhakikisha wanazipitia kodi zote.

Wanaangalia zipi zina manufaa kwa serikali, zile ambazo ni nyingi, ni utitiri, wanaweza wakaziunganisha. Lengo ni kuwa na kodi rafiki ili walipakodi walipe kirahisi bila kuwapo usumbufu. Ni eneo ambalo tunaliangalia kwa undani zaidi.

**SWALI: Ulisikika pia ukitamka kwamba wewe siyo muumini wa 'kufukua makaburi'. Kauli hii ina maana gani hasa?**

**RAIS MWINYI:** Ninachokusudia hasa ni kwamba, kuna mambo ambayo yalifanyika siku za nyuma ambayo kimsingi hayakuwa sahihi. Sasa, badala ya kuanza kutafuta mambo ya siku nyingi nyuma, yatatuondoa katika mstari wa kutazama mbele.

Mimi ninapenda zaidi tuanzie hapa tulipo twende mbele. Kwa hiyo, hayo ya nyuma yasituchukulie muda mwingi wa kutafutana.

Na kwa maana hiyo ninaamini kwamba kama wamenielewa, maana yake ni kwamba wale waliokwepa kodi, sasa hawatafanya hivyo tena. Kwa hiyo, ninaamini kwamba wale wote waliokuwa na ubadhirifu na wizi katika taasisi za serikali, wataacha mara moja tabia hiyo.

**SWALI: Je, tafsiri ya hili ni kwamba kama kuna mtu alikuwa anadaiwa kodi na serikali, umemsamehe?**

**RAIS MWINYI:** Unajua, ninachomaanisha ni kwamba ukienda kudai kodi ya miaka mitano iliyopita, huenda isikupe tija kama kuanza sasa kufanya hivyo.

Ninachokizungumza sasa ni kwamba tuwajibike zaidi kuanzia sasa kwenda mbele na kuondoa utaratibu wa kutafuta mengi yaliyotokea huko nyuma, kwa sababu siyo suala la kodi tu, huko nyuma yalitokea mambo mengi tu ambayo ndani yake kuna wizi, kuna ubadhirifu, kuna mambo ambayo hayakuwa sawasawa.

Njia bora zaidi, badala ya kutafutana kwa yaliyotokea miaka mingi nyuma, kwanini tusianze sasa hivi tukarekebisha mstari unyoke kila mtu atimize wajibu wake?

**SWALI: Tangu uingie madarakani, umekuwa ukisisitiza nidhamu ya utumishi. Ufisadi ulioubaini Zanzibar, uko katika maeneo yapi hasa?**

**RAIS MWINYI:** Ufisadi kwa kweli zaidi uko kwenye taasisi ambazo ziko chini ya serikali; kwenye wizara, kwenye idara, kwenye mashirika ya umma na kadhalika.

Hata kwenye sekta binafsi ufisadi upo kwa sababu kuna watu wanakwepa kodi, kuna watu hawawajibiki kwenye maeneo yao.

Pengine, wakati sasa umefika wa kuhakikisha kila mtu anawajibika, anaondoa masuala ya ubadhirifu na wizi wa mali ya umma na kila mmoja wetu anakuwa na wajibu wa kulipa kodi kwa maendeleo ya nchi yetu.

**SWALI: Umeanza kwa kasi kubwa. Mtaani wanasema 'kasi ya 4G'. Nini siri ya hili?**

**RAIS MWINYI:** ... (kicheko kidogo) Ni kwa sababu tu kwamba tumechelewa. Kwa maana hiyo, wakati wenzetu wanatembea, sisi lazima tukimbie. Na ndiyo maana tunaona kuna kila sababu ya kuweka spidi ya aina yake ili kutimiza matarajio ya wananchi walio wengi ambao kwa kweli wana matumaini makubwa.

Kwa hiyo, nimeona kama kiongozi wa juu nionyeshe mfano kwa viongozi wengine niliowateua, kwa kuwa na spidi kubwa ya kufanya uamuzi ili kuleta maendeleo.

Lengo ni kuhakikisha kuwa wakati tunamaliza kipindi chetu cha miaka mitano, tuwe tumetimiza yale ambayo wananchi wanayatarajia kutoka kwetu.

**SWALI: Spidi hii unayokwenda nayo, inaeleweka kwa Wazanzibar?**

**RAIS MWINYI:** Kwa kweli ni jambo jipya, lakini ni jambo ambalo linazoeleka. Tumeanza tunasukumana na ni mategemeo yangu baada ya muda mfupi tutakuwa tumeelewana na sote tutakuwa tunakwenda kwa spidi moja.

**SWALI: Nini siri ya kukutana na makundi mbalimbali ya watu maana hata kwenye kampeni zako ulitumia staili hii?**

**RAIS MWINYI:** Mimi ni muumini sana wa mawazo ya wadau na ninaamini kwamba katika kila sekta ukizungumza na wadau, utapata kila changamoto, utapata na ushauri wa uamuzi wa kuchukua.

Tumekutana na wadau wa sekta ya afya, tumekutana na wadau wa sekta ya elimu, tumekutana na wadau wa masuala ya wazee. Yote hiyo ilikuwa katika kutafuta maoni, wao wanaonaje na wanatushauri nini?

Kwa kweli nimefarijika kwa sababu tumepata mawazo mengi sana ya utendaji, mawazo ambayo tukiyatimiza, tutakuwa tumefanya mabadiliko makubwa katika sekta hizo nilizozitaja.

Nilikutana pia na wadau wa masuala ya udhalilishaji. Na wenyewe walitoa maelezo ya kina wanachotaka na ni mambo gani wanahisi yakifanyika, hili jambo tutalirekebisha. Kwa hiyo, mimi ni muumini wa kusikiliza watu wanachotaka na wao wanao ufumbuzi wa mambo mengi.

**SWALI: Mara kadhaa katika mikutano yako umekuwa ukisisika ukisema hautakuwa na muhali na mtu yeyote. Unalenga kufikisha ujumbe gani hasa?**

**RAIS MWINYI**: Ni tatizo hapa Zanzibar. Nianze kwa kusema maana ya neno lenyewe -- muhali maana yake ni kuoneana aibu, kuoneana haya... eeh! Kutotaka kuchukua hatua dhidi ya mtu unayemjua.

Unajua Zanzibar ni ndogo na katika kila eneo kuna mtu atakuwa ni ndugu yako, mwanao, shemeji, rafiki. Kutokana na huo ukaribu wa watu, basi wanaofanya makosa ilikuwa shida kuwachukulia hatua.

Sasa, mimi nilitangaza tangu mapema kabisa kwamba kwa kweli suala la muhali tutaliweka pembeni ili mambo yakae sawasawa. Na hilo ndilo lililofanya, niliwatahadharisha mapema kwamba tutawagusa watu ambao tuna undugu nao. Ni jambo ambalo kwa kweli lilihitaji kuchukuliwa hatua.

**SWALI: Tatizo la wizi wa dawa lipo hapa Zanzibar? Kama lipo, hatua gani zinachukuliwa kulitatua?**

**RAIS MWINYI:** Tatizo lipo. Wizi wa dawa upo Zanzibar, lazima tukiri. Moja ya ufumbuzi wa matatizo ni kukiri uwapo wake. Kuna dawa ambazo katika ununuzi, hazifiki kwenye vituo vinavyotakiwa na zile zinazofika, zinapungua kutokana na wizi wa aina mbalimbali.

Hatua tunazozichukua ni pamoja na kuhakikisha watu wanawajibika. Pale tunapomgundua mtu anafanya vitendo hivyo, basi tunachukua hatua za haraka. Pia tunapanga utaratibu mzuri zaidi kwamba dawa za serikali ziwe na alama fulani ili zitambulike kirahisi.

*ITAENDELEA KESHO

# Adaiwa kuwachoma kisu watoto kisa mke kuolewa na mwingine

**Na Alphonce Kabilondo,**
GEITA

JACKSON Bahati (27), mkazi wa kijiji cha Buhangizi, Kata ya Kagu, mkoani Geita, anadaiwa kuwajeruhi watoto wake wawili kwa kuwachoma kisu maeneo ya tumboni baada ya kwenda kijiji jirani na kumkuta mke wake ameolewa na mwanamume mwingine.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Geita, Kamishna Msaidizi (ACP) Dismas Kisusi, akithibitisha jana tukio hilo amesema kuwa tukio lilitokea majira ya saa 9:00 usiku Januari 27, mwaka huu.

Alisema baada ya kutenda kitendo hicho, mtuhumiwa naye alijichoma kisu mara nne kwenye tumbo lake na kisha kunywa sumu ya panya kwa lengo la kujiua.

Kamanda Kisusi aliwataja watoto waliojeruhiwa kuwa ni Leah Jackson (4) na Bahati Jackson (3) ambao wote walichomwa kisu maeneo ya tumboni na baada ya kutokea kwa tukio hilo, walipata msaada kutoka kwa raia wema na kupelekwa Hospitali ya Nzera na hadi sasa hali zao zinaendelea vizuri.

Kisusi alisema mtuhumiwa huyo akiwa chini ya ulinzi wa polisi, aliwahishwa na askari katika Hospitali ya Nzera na baadaye kuhamishiwa katika Hospitali ya Wilaya Sengerema mkoani Mwanza ambako mpaka sasa anaendelea kushikiliwa na polisi ili sheria ichukue mkondo wake.

"Chanzo cha tukio hilo ni mgogoro wa kifamilia ikiwa ni baada ya mama watoto, ambaye ni mke wa mtuhumiwa kutoroka nyumbani kwake na kuacha watoto hao na kwenda kusikojulikana. Baada ya baba watoto kumtafuta bila mafanikio ndipo akachukua uamuzi huo," alisema.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Mkoa wa Geita, Last Lingson, alisema ili kuzuia matukio ya aina hiyo yanayotokana na usaliti na migogoro ndani ya familia, ni vyema wanandoa wajaribu kuangalia namna ya kuzuia viashiria hatarishi vinavyoweza kusababisha usaliti ndani ya ndoa.

Last aliwashauri watu ambao wako kwenye maumivu yanayotokana na migogoro ya ndoa kuwashirikisha wanasaikolojia au marafiki wa karibu mapema ili kuepuka kuchukua uamuzi unaoweza kuwagharimu ikiwamo kujiua na kufanya vitendo vya ukatili kwa ndugu zao wa karibu.

# Kortini madai kulawiti mtoto wa miaka mitatu

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MKAZI wa Kijiji cha Ibisabageni, Masanja Ndalawa (53), amefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Geita kwa tuhuma za kumlawiti mtoto wa kiume mwenye umri wa miaka mitatu na kumsababishia maumivu makali sehemu za haja kubwa.

Mshtakiwa huyo alifikishwa mahakamani hapa jana majira ya saa 3:00 asubuhi na kupandishwa kizimbani majira ya saa 7:00 mchana mbele ya Hakimu Mkazi Sosthenes Kiiza. Aliposomewa shtaka lake alikana na yuko ndani kwa kukosa wadhamini.

Upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali, Clemence Kato, ulidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo umekamilika na kuomba tarehe kwa ajili ya kumsomea mshtakiwa huyo maelezo ya awali.

Hakimu Kiiza alikubaliana na ombi hilo na kuahirisha hadi Febuari 17, mwaka huu, kwa ajili ya kumsomea mshtakiwa maelezo ya awali.

Hakimu Kiiza aliyataja masharti ya dhamana kwa mshtakiwa kuwa na wadhamini wawili wenye barua ya utambulisho kutoka kwa ofisa mtendaji wa kata pamoja na kitambulisho cha Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) na mali isiyohamishika yenye thamani ya Sh. milioni 10.

Hata hivyo, mshtakiwa alishindwa kutimiza masharti hayo na hakimu kumtaka kwenda mahabusu katika Gereza la Geita.

Akisoma hati ya mashtaka, Wakili Kato alidai kuwa Desemba 17, mwaka jana, katika Kijiji cha Ibisabageni Kata ya Isulwadutundwe, Mkoa wa Geita, mshtakiwa alimlawiti mtoto wa kiume mwenye umri wa miaka mitatu na kumsababishia maumivu makali sehemu za haja kubwa, kitendo ambacho ni kinyume cha sheria.

# PM ataka mifuko ya uwezeshaji kuboresha masharti ya mikopo

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameiagiza mifuko na programu zote za uwezeshaji ifanye tathmini ya shughuli na huduma zake ili kubaini mafanikio, changamoto na maeneo yanayohitaji uboreshaji hususan eneo la masharti ya utoaji mikopo kwa wajasiriamali.

Pia ameitaka mifuko inayotoa dhamana kwa wafanyabiashara na wajasiriamali iimarishe usimamizi, uratibu na utendaji wake kwa kutengeneza mipango maalum ya kila mwaka inayoonesha malengo ya dhamana zitakazotolewa katika mwaka husika.

Alitoa maagizo hayo jana wakati wa ufunguzi wa Maonesho ya Nne ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji Wananchi yanayoendelea jijini Arusha, na kwamba Serikali inataka mikopo itolewe kwa masharti nafuu zaidi na riba ndogo kuliko ilivyo sasa.

WaterAid



Shirika la WaterAid tunapenda kumtambulisha kwenu Mrs. Anna Tenga Mzinga kama Mkurugenzi Mkaazi mpya wa shirika la WaterAid Tanzania kuanzia mwezi Januari, 2021. Anna Tenga Mzinga amekuwa akikaimu nafasi ya Mkurugenzi Mkaazi kwa miezi saba iliyopita na ana uzoefu wa zaidi ya miaka 20 katika uongozi wa juu kwenye mashirika ya umma, vyuo vya elimu ya juu na katika mashirika yasiyo ya kiserikali.

WaterAid ni shirika la kimataifa lisilo la kimaslahi linalofanya kazi zake katika nchi 34 duniani (zikiwemo nchi 18 za Afrika) na kubadili maisha ya wananchi wenye kipato cha chini kwa kuwafikishia huduma ya maji safi na salama, vyoo bora na usafi wa mazingira.

Shirika la WaterAid linafanya kazi na wadau, sekta binafsi, taasisi na mashirika ya kiserikali, ikiwa ni mbinu ya kufikia lengo la upatikanaji wa huduma za maji na mazingira safi kwa kila mtu na kila mahali ifikapo mwaka 2030.

Tunaamini kupitia uongozi wake shirika hili litaweza kufikia malengo yake hapa Tanzania kuhakikisha kila mmoja anafikiwa na maji safi na huduma za usafi wa mazingira zilizoboreshwa kufikia mwaka 2030.

Shirika linampongeza sana na kumtakia kheri Mrs. Anna Tenga Mzinga anapochukua nafasi hii ya uongozi hapa Tanzania.

Olutayo Bankole-Bolawole
Mkurugenzi, Afrika Mashariki
WaterAid

@wateraid_tanzania @WaterAidTZ https://www.wateraid.org/tz

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tusijisahau mvua hii

**MVUA** imeanza kunyesha sehemu mbalimbali ikwa ni pamoja na Dar es Salaam, japo haijaelezwa kuwa imekatiza shughuli za wananchi hasa usafiri na usafirishaji ni wakati wa kuanza kuchukua tahadhari.

Ni kawaida kuona shughuli mbalimbali zikiwamo za usafirishaji zikitatizwa hasa mabasi ya mwendokasi ambayo mara kadhaa yanazuiliwa kutumia njia ya Morogoro inayokatisha Jangwani, kutokana na mvua kubwa.

Lakini, tunachopenda kuzungumzia kuanzia sasa ni kuchukua tahadhari kukabili uharibifu wa maisha na mali yakiwamo makazi unaotokana na mvua.

Wakati mwingine mvua haionyeshi dalili ndiyo maana tunaona kuwa kuna haja ya watu kuchukua tahadhari mapema kuepusha maafa.

Jijini Dar es Salaam, vifo, kuharibu makazi, mali na miundombinu si jambo geni ni tatizo linalojirudia mara kwa mara.

Mafuriko kwenye makazi hasa ya wanaoishi mabondeni, kwenye mikondo ya maji na sehemu ambazo ujenzi umeziba njia za maji umechangia kujeruhi na kuangamiza maisha ya watu.

Ni mambo ambayo licha ya kuwakasirisha wananchi wengi hasa waathirika, hayajapata ufumbuzi endelevu na kila mwaka.

Tuchukue hatua kwani mvua itaendelea kunyesha na kama hatutajali maisha yetu itaendelea kutuachia adha kubwa.

Ikumbukwe kuwa mambo yanakuwa magumu wakati mvua kubwa inapoanza kunyesha kuanzia alfajiri hadi jioni au usiku kucha.

Ingawa ujenzi wa miundombinu unaendelea na barabara zimepanuliwa na kuwa za kisasa zinazoendelea kujengwa pamoja na kuwapo kwa mitaro ya kusafirisha maji ya mvua na majitaka ukweli ni kwamba bado jiji haliko salama na mafuriko.

Ni wazi kuwa barabara kadhaa kama ya Morogoro wakati wa mvua inakwama kuwa kiunganishi hasa sehemu ya Jangwani, hivyo kuwa kikwazo cha kuyafikia maeneo kadhaa na katikati ya jiji.

Wakazi wa mabondeni na kwenye mikondo na majirani wa Mto Msimbazi, wakumbuke maji yanaweza kuujaza Msimbazi hata bila kunyesha Dar hivyo wajihadhari zaidi.

Inaonyesha kuwa mvua inayonyesha Kisarawe inasababisha mafuriko Jangwani na maeneo jirani ya Mto Msimbazi kwa sababu sehemu kubwa hujaa maji ambayo pia hushuhudiwa sehemu nyingine hasa Mkwajuni na kwenye mito mikubwa ya Dar.

Mvua za wakati huu ni za mabadiliko ya tabianchi, zinaambatana na tufani na maporomoko ya udongo ni vyema kuchukua tahadhari hasa wakazi wa milimani wanaoishi jijini Mwanza.

Hali inatajwa kuwa inakuwa mbaya zaidi iwapo milima inaporomoka na kufukia makazi pamoja na kuangamiza maisha ya watu.

Si kwamba tunawatishia watu kwa vile nyakati nyingine wanategemea kusikia taarifa za kuelekezwa kuchukua tahadhari kutoka Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA), ukweli ni kwamba mvua hii si ya kupuuza.

Tunazikumbusha kamati za maafa za mikoa na wilaya kuwa na mipango ya kukabiliana na hali hiyo badala ya kusubiri hadi madhara yanapotokea.

Kwa kipindi hiki ambacho mvua haijaleta athari ni vyema kuwa makini zaidi na kuweka mikakati ya namna bora ya kuwasaidia watu endapo maafuriko na maafa yatatokea.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com



## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# 'Vijana msiendelee kuwa taifa la kesho'

KUWAITA vijana kuwa ni taifa la kesho ni msemo uliozoeleka na ndilo jeshi linalotumiwa na wanasiasa kwa kuwa karibu nao kuwaelimisha na kuwandaa kwa ajili ya kushika nyadhifa mbalimbali za uongozi baadaye.

Mbali na kubatizwa taifa la kesho, wanaoaminiwa kuwa ni nguvukazi ya taifa kwa kuwa wana nguvu nyingi na ni wepesi katika kufanya kazi kutokana na umri na uwezo wao mkubwa kuchapa kazi.

Kwenye uwanja wa siasa vijana ndiyo wanaoving'arisha vyama na kuonekana kuwa na nguvu, kutokana na hamasa zao zinazovifanya viwe maarufu popote wanapovisimamia.

Lakini pamoja na juhudi hizo, kuvisaidia vyama vya siasa, baadhi yao hujikuta wakitumiwa vibaya na viongozi wa vyama hivyo ikiwamo kuanzisha vurugu kwa manufaa ya wanasiasa wachache.

Wengine ushiriki wao katika masuala ya kijamii huwa ni hafifu, na inawezekana ni kutokana na kutoandaliwa vyema na kubaki kutumika tu kufanya yasiyofaa kwa manufaa ya wengine.

Kwa hali kama hiyo ni wazi kwamba, lengo la kuwa karibu na wanasiasa au kujiunga na vyama ili waandaliwe kushika nafasi mbalimbali za uongozi hao baadaye, linakuwa halijatimia.

Umefika wakati sasa wajiongeze na kukataa kutumika kwa manufaa ya watu wachache, bali wapime malengo ya wanasiasa, na iwapo hayalengi kuwandaa kushika uongozi, basi waachane nao.

Wanasiasa wana ushawishi katika kuelezea matatizo ya vijana, lakini baadhi yao hujikuta wakigeuzwa kuwa madaraja ya wanasiasa hao wasio na lengo la kuwaandaa kuwa taifa la kesho.

Iwapo wanasiasa wameshindwa kuwandaa kushika nafasi za uongozi hapo baadaye, vijana wenyewe watafute njia nyingine halali ambazo zitawawezesha kufanya shughuli zao ili kukwepa wanasiasa wasio na nia njema.

Kuna dhana kwamba, mara nyingi vijana huwa wanaojitokeza kushiriki maandamano, na mikutano ya hadhara ya kisiasa wanadaiwa kufanya hivyo kwa sababu hawana shughuli za kufanya, hivyo, ni vyema sasa vijana wakaliona hilo na kutafuta njia nyingine ambayo inaweza kuwaepusha kujiingiza kwenye mambo ambayo yanaweza kuwafanya waonekane hawana maana mbele ya jamii.

Wasiwachukulie wanasiasa na siasa kama suluhisho la matatizo yao, bali iwe ni sehemu ya kuandaliwa kuwa viongozi bora wa baadaye, na hilo lisipoonena ni bora wakaachana na siasa kuliko kujihusisha na vurugu.

Hakuna umuhimu kwa vijana kukimbilia kujiunga na vyama vya siasa ambavyo hawaandai kuwa viongozi na badala yake kubaki kushabikia mambo ambayo yanaweza kusababisha wasifike kokote kisiasa.

Dhamira za kisiasa ni ukombozi wa kifikra, usawa wa binadamu na nafasi ya mwanamke na mwanaume katika uongozi, wakiwamo vijana, hivyo wanasiasa wawaandae vijana kuwa taifa la kesho.

Ikumbukwe kuwa taifa kufanikiwa siku za usoni, hutategemea juhudi na uwepo wa vijana katika kushirikisha kwenye uongozi na mipango ya maendeleo na siyo kuwatumia vibaya wakati wa kampeni za kisiasa.

Siyo vibaya vijana wakakataa dhana ya kwamba wao ni taifa la kesho, badala yake wapewe nafasi za uongozi kuliko kuendelea kutumiwa kama madaraja ya kuvusha wasiasa kufanikisha malengo yao.

Kutowaandaa vijana ni kupuuza taifa la leo na kesho ni kupuuza maendeleo, hivyo wale ambao wamekuwa wakiwatumia kama madaraja, watambue kuwa wanakwamisha taifa la kesho.

Iwapo vijana wanadhani kwamba wanaminywa katika vyama vya siasa waanzishe mjadala wa kuwapo kwa mgombea binafsi, wawe huru ili hata wale wasio katika vyama waweze kuwania nafasi za uongozi.

Mfumo huo wa mgombea binafsi unaweza kuondoa ukiritimba wa watu kuchaguana kwenye vyama kwa kujuana na kupitishwa bila kupingwa, huku wenye uwezo wa kuongoza wakiachwa na kukomolewa.

Hivyo vijana hawana budi kujiongeza wenyewe kwa kuliona hilo na kushawishi kuwapo mgombea binafsi, ili kupata viongozi zaidi, ambao baadhi yao wana uwezo wa kuongoza, lakini si wanasiasa.

# Amri ya serikali yawapeleka shule watoto wa mchungaji

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

HATIMAYE watoto waliozuiwa kwenda shule na baba yao ambaye ni mchungaji, wameanza masomo katika Shule ya Msingi Buyekera iliyopo Manispaa ya Bukoba mkoani Kagera, kwa amri ya serikali.

Serikali imeamua kutumia nguvu kuhakikisha watoto wa mchungaji huyo aliyeripotiwa kuzuia watoto wake kwenda shule wanaanza masomo.

Mkuu wa Wilaya wa Bukoba, Deodatus Kinawilo, aliyefika kwenye familia hiyo Februari 3, mwaka huu, kujionea hali halisi, aliagiza watoto hao kupelekwa shule.

Wanafunzi hao wanatoka katika familia ya mchungaji huyo inayoamini kuwa elimu ya dunia haitambuliki katika maandiko ya vitabu vya dini.

Mchungaji huyo, Malchades Buberwa na mkewe, Aglipina Pius, walizuia watoto wao kwenda shule kutokana na imani wanayoamini.

Mkuu wa shule hiyo, Jacob Kaijage, akizungumza na waandishi wa habari vilivyofika shuleni hapo, alisema kutokana na umri wa wanafunzi hao kila mmoja amepangiwa darasa lake.

"Joseline Buberwa (13) yeye kwa vile umri wake ni mkubwa ataingia darasa la MEMKWA ili wafanye mtihani wa darasa la nne na ikionekana kufanya vizuri, ataombewa kuingia darasa la sita.

Mwanafunzi mwingine, Joshua Buberwa anaingia darasa la pili kulingana na uelewa wake kwa kuwa anajua kusoma na kuandika na Anna Buberwa anaanza darasa la awali," alisema Kaijage.

Mama wa wanafunzi hao, Aglipina Pius, alisema hajafurahishwa na kitendo cha watoto wake kwenda shule, isipokuwa ameamua kuiheshimu serikali.

"Sijafurahishwa kwa sababu ya kifungu cha torati...Mungu wangu ni mkali sana, sitanena lolote juu ya hilo bali nyamaza kimya yeye asimame," alisema.

Ofisa Elimu Shule za Msingi Manispaa ya Bukoba, Dk. Elpidius Bagonza, alisema ataendelea kuongea na wazazi, viongozi wa dini kuhakikisha wanafunzi hao wanahudhuria shuleni.

# Mpango waiva sekta ndogo ya fedha

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

OFISI ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) imefanya uteuzi wa watu 212 katika ngazi za wizara, mikoa na halmashauri kwa ajili ya uratibu na uhamasishaji wa biashara ya huduma ndogo za fedha nchini.

Pia serikali tayari imeandaa kanuni mahususi zitakazotumika kwa ajili ya usimamizi na udhibiti wa sekta hiyo, pamoja na kanuni za jumla kutekeleza majukumu ya waziri ya kisera ikiwa ni pamoja na kuhamasisha, kusimamia na kuendeleza sekta hiyo.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Adolf Ndunguru, alibainisha hayo jana jijini hapa alipokuwa akifungua mafunzo ya waratibu wa biashara ya huduma ndogo za fedha.

Alisema majukumu ya waratibu hao ni kuratibu, kuhamasisha na kutathmini biashara ya huduma ndogo za fedha katika ngazi za wizara, mikoa na halmashauri ikiwa ni pamoja na kusajili wahamasishaji wa biashara ya huduma ndogo za fedha na kuandaa taarifa za sekta ndogo ya fedha kwa vipindi tofauti.

Kadhalika, alisema sekta ndogo ya fedha ni miongoni mwa sekta muhimu katika uchumi wa nchi.

"Sekta hii inatoa huduma za fedha kwa wananchi wa kipato cha chini kwa lengo la kuongeza kipato na kuchangia katika kukuza uchumi," alibainisha Ndunguru.

Alisema, kwa mujibu wa utafiti wa Finscope wa mwaka 2017, asilimia 55.3 ya nguvu kazi ya taifa wanapata huduma za fedha kutoka taasisi za huduma ndogo za fedha.

Pia alisema kutokana na umuhimu wa sekta hiyo, serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango ilifanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2000 na kutunga Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2017 pamoja na mkakati wa utekelezaji wake kwa kipindi cha miaka kumi kuanzia 2017/18 mpaka 2027/28.

Pia alisema sera hiyo pamoja na mambo mengine, ilielekeza kutungwa kwa sheria mahsusi ya kusimamia na kuendeleza sekta ya ndogo ya fedha ili kuondoa changamoto za kisheria zilizokuwapo ambazo ziliathiri usimamizi, udhibiti na ustawi wa sekta hiyo.

"Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na taasisi za huduma ndogo za fedha kutoa mikopo kwa wananchi kwa vigezo na masharti magumu na hivyo kusababisha madhara kwa wananchi ikiwa ni pamoja na viwango vikubwa vya riba na tozo, kukosekana kwa uwazi wa masharti ya mikataba ya mikopo, utoaji holela wa mikopo ambao unasababisha limbikizo la madeni kwa wateja," alisema Ndunguru.

Vile vile, alisema sababu nyingine ni utaratibu usiofaa wa ukusanyaji wa madeni ambao unasababisha wananchi kupoteza mali zao pia kuwapo kwa baadhi ya taasisi za huduma ndogo za fedha zisizotoa gawio au faida kwa wanachama au wateja wanaoweka fedha kati ya asilimia 25 hadi 30 kama dhamana ya mikopo.

"Changamoto nyingine ni ukosefu wa takwimu/taarifa sahihi za uendeshaji wa taasisi za watoa huduma ndogo za fedha na hivyo serikali kutojua mchango wa sekta ndogo ya fedha katika uchumi wa taifa, ukosefu wa utaratibu wa kuwalinda watumiaji wa huduma ndogo za fedha na kuwepo kwa mianya ya utakasishaji wa fedha haramu kutokana na taasisi za huduma ndogo za fedha kutokuwa na utaratibu wa kisheria unaozitaka kutekeleza matakwa ya Sheria ya Udhibiti wa Utakasishaji wa fedha haramu," alisema Ndunguru.

Alisema ili kutatua changamoto zinazoikabili Sekta Ndogo ya Fedha serikali ilitunga Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2018 (The Microfinance Act, 2018) ili pamoja na mambo mengine ni kuzitambua taasisi za huduma ndogo za fedha katika madaraja manne.

"Daraja la kwanza ni taasisi za huduma ndogo za fedha zinazopokea amana (deposit taking microfinance providers), Daraja la Pili, taasisi za huduma ndogo za fedha zisizopokea amana (non-deposit taking microfinance service providers) wakiwamo wakopeshaji binafsi, watoa huduma kwa njia ya kielektroniki.

"Daraja la Tatu, Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) na Daraja la Nne ni vikundi vya kijamii vya huduma ndogo za fedha kama vile VICOBA, VSLA," alifafanua Ndunguru.



Meneja Mwandamizi Idara ya Biashara za kadi wa Benki ya NMB, Manfred Kayala (katikati), akifafanua jambo kwa waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, wakati wa droo ya tisa ya NMB MastaBata siyo Kikawaida. Kushoto ni Ofisa kutoka Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania, Joram Mtafya na Ofisa Huduma kwa Wateja, Neema Deus Kazoviyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mfanyakazi DAWASA ahukumiwa kwa rushwa

**Na Julieth Mkireri, KIBAHA**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Pwani imemfikisha mahakamani Gidma Athanas, mtumishi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) kwa tuhuma za kuomba na kupokea rushwa.

Kitendo hicho, kimedaiwa kuwa ni kinyume cha kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya mwaka 2007.

Suzana Raymond, Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Pwani, alisema jana kuwa mtuhumiwa huyo aliomba rushwa ya Sh. 220,000 kutoka kwa mwananchi, mkazi wa Kibaha Picha ya Ndege ili asiingize deni la matumizi ya maji la Sh. 500,000 kwenye mfumo wa malipo ya DAWASA.

Raymond alisema baada ya mtuhumiwa kufikishwa mbele ya Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Wilaya ya Kibaha, Fahamu Kibona, alisomewa mashtaka na kukiri kutenda kosa.

Kutokana na kukiri huko, mtuhumiwa alihukumiwa kwenda jela miaka mitatu au kulipa faini ya Sh. 500,000 ambayo alilipa na kuachiwa huru.

Wakati huo huo, TAKUKURU Wilaya ya Mkuranga, Novemba, 2019, ilifungua mashtaka ya kuomba na kupokea rushwa dhidi ya Juma Abeid aliyekuwa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya hiyo.

Raymond alisema kesi hiyo iliendeshwa mbele ya Hakimu Mkazi Herieth Mwailolo.

Ilidaiwa mahakamani hapo kuwa mshtakiwa alitenda kosa la kupokea hongo kumsaidia mwananchi aliyekuwa akihitaji uhamisho wa mke wake, ambaye ni mwalimu kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Babati mkoani Manyara kwenda Mkuranga.

Ilidaiwa kuwa mshtakiwa aliomba na kupokea Sh. 220,000 ili kuwezeaha uhamisho huo kitendo ambacho ni kosa chini ya kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya mwaka 2007.

Hukumu ya kesi hiyo iliyosomwa na Hakimu Mwailolo, mtuhumiwa alihukumiwa kwenda jela miaka minne au kulipa faini ya Sh. 700,000 kwa kila kosa na alikubali kulipa faini ya Sh. 1,400,000 kisha kuachiwa huru.

# Bil. 16.4/- zamwagwa maji Songwe

**Na Thobias Mwanakatwe**

MKOA wa Songwe umepata Sh. bilioni 16.4 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa maji vijijini kupitia Mpango Maalum wa Lipa kwa Matokeo (PfoR) unaotarajia kuanza hivi karibuni.

Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Brigedia Jenerali Nicodemus Mwangela, alisema jana kuwa miradi hiyo itakapokamilika itasaidia kuongeza upatikanaji wa maji vijijini kutoka asilimia 73 hadi asilimia 100.

"Nitoe wito kwa jamii kutunza vyanzo vya maji na kuilinda miradi ili wananchi wapate maji kwa muda mrefu," alisema Mwangela.

Naye Meneja wa Wakala wa Usambazaji Maji Vijijini (RUWASA) Mkoa wa Songwe, Mhandisi Charles Pambe, alisema utekelezaji wa miradi ya maji kupitia 'Force Account' umesaidia kuwajengea uwezo wataalamu kutekeleza miradi kwa asilimia 100.

Pambe alibainisha kuwa RUWASA imejipanga kutekeleza miradi hiyo ndani ya miaka mitatu ili vijiji vyote visivyokuwa na maji katika mkoa wa Songwe vianze kutoa maji.

Alisema mkoa ulipata Sh. bilioni 5.6 za PfoR kama mbegu kwa ajili ya utekelezaji wa miradi, lakini kutokana na mkoa kufanya vizuri kwenye utekelezaji, zimezalishwa tatu hadi kufikia Sh. bilioni 16.4.

# Vijana watakiwa kutumia mitandao ya jamii kibiashara

**Na Onesmo Andrea,** SJMC

VIJANA wameshauri kutumia mitandao ya kijamii kutafuta masoko ya bidhaa zao na kuwafikia wateja kirahisi zaidi, jambo ambalo litapunguza malalamiko ya ukosefu wa ajira.

Ushauri huo ulitolewa jijini Dar Es Salaam na vijana wanaofanya biashara kwa njia ya mtandao, ambao walisema mitandao imesaidia kuwafikia wateja kirahisi zaidi na kuongezea wigo wa ajira.

"Maisha siyo mepesi, maisha ni kupambana na kama una ndoto au malengo ya kufanikiwa huwezi kukaa nyumba ukisubiri kuajiriwa bali unatakiwa kujaribu kufanya kitu kingine ikiwamo biashara yoyote," alisema Kelvin Amanzi.

Amanzi ambaye anauza nguo na viatu katika eneo la Sinza, alisema vijana wanatakiwa kujishughulisha katika shughuli mbalimbali pamoja na kuitumia mitandao ya kijamii kwa ajili ya kujiongezea kipato ili kuendesha maisha yao.

"Siku hizi teknolojia nimekuwa ninatumia mitandao ya Facebook, WhatsApp, Instagram katika kutangaza bidhaa zangu ili kuwafikia wateja wangu," alisema.

Alisema alianza biashara yake kwa mali kauli kikubwa kinachohitajika ni heshima na uaminifu kwa watu ili kufikia malengo katika biashara.

# Mgawanyo wilaya wawagawa madiwani

**Na Anthony Gervas,** MAGU

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Magu mkoani Mwanza, wameshindwa kufikia mwafaka wa mapendekezo ya kugawa wilaya mpya ya Kisesa, hivyo kufanya mchakato huo kuwa njia panda.

Katika kikao hicho kilichofanyika hivi karibuni, baadhi ya madiwani walipendekeza mpaka wa wilaya hiyo kuishia kijiji cha Ngashe, Kata ya Kitongosima huku baadhi wakitaka uwe katika kijiji cha Matela hali iliyosababisha kukosekana mwafaka.

Diwani wa Bukandwe, Marco Minze, alisema katika kikao cha kamati ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kilipofanyika, wajumbe walitoa mapendekezo yao na kwamba asilimia kubwa walipendekeza mpaka uwe katika kijiji cha Ngashe.

"Katika kikao cha kamati tulipiga kura za ndiyo, kura 20 zilishinda dhidi ya 28 za wajumbe zilizopigwa kuwa mpaka uwe kijiji cha Ngashe halafu jimbo liitwe Bujora na makao makuu yawe Kata ya Bukandwe," alisema Minze.

Licha ya mvutano huo kuwapo kwa madiwani hao, baadhi waliunga mkono mapendekezo ya wataalamu wa serikali waliotaka wilaya hiyo mpya mpaka wake uwekwe katika kijiji cha Matela.

Hatua ya kuanzishwa kwa Wilaya ya Kisesa imetokana na tamko la Rais John Magufuli alipokuwa katika kampeni za uchaguzi mkuu mwaka jana baada ya kufika katika miji midogo ya Kisesa na Igoma na kushuhudia kuwapo maelfu ya wananchi.

Mkuu wa Wilaya ya Magu, Salum Kali, aliwataka madiwani kuacha mvutano katika suala hilo ambao hautakuwa na faida kwa wananchi bali waweke mawazo pamoja kwa ajili ya kuleta maendeleo ya wananchi na taifa.

Kali alisema wao ni kioo cha jamii, hivyo wanatakiwa kushikamana badala ya kutofautiana kwani hakuna hasara yoyote katika kuwekwa mpaka wake.


halotel




Royal

Ishi kifalme

Piga *148*66#

| Kiasi | Halotel-Halotel (dk) | Mitandao yote (dk) | SMS | Intaneti (GB) | Muda |
|---|---|---|---|---|---|
| 10,000 | 400 | 150 | 500 | GB 7 | Siku 30 |
| 20,000 | 800 | 300 | 500 | GB 15 | Siku 30 |
| 30,000 | 1,000 | 400 | 500 | GB 23 | Siku 30 |
| 40,000 | 1,500 | 500 | 1,000 | GB 31 | Siku 30 |
| 50,000 Tanzanite | Dk 200 kila siku | | 1,000 | GB 40 | Siku 30 |

halotel_tanzania halotel Tanzania



WAUNGWANA AUCTION MART LTD

P.O.BOX 75966 DAR ES SALAAM
Mob: +255 713077474/ +255 717 023 338+255 718545519
Email: waungwana2017@gmail.com

**NOTISI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kwa mamlaka tuliyopewa na **LETSHEGO BANK (T) LTD** tutauza kwa njia ya mnada wa hadhara nyumba/magari/viwanja vya wadaiwa wa bank ya **LETSHEGO (T) LTD** vilvyowekwa Kama dhamana ya mkopo ambapo wateja husika wameshindwa kulipa mikopo yao kwa mujibu wa mikataba husika. Mnada utafanyika kuanzia saa 4 asubuhi na kuendelea:

| S/N | JINA LA MTEJA | JINA LA MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| i. | PROJESTUS PROSPER TIMANYIKA | MSAFIRI MICHAEL NYARUGA | NYUMBA | NYAKATO SOKONI - MWANZA | 15/2/2021 |
| ii. | OMARI MOHAMED ATHUMANI | JACOB STEPHEN LAISSER | NYUMBA | MWAMALA KATA YA MASEKELO - SHINYANGA | 17/02/2021 |
| iii. | SELEMANI L. MAGUHA | ROBERT CHRISTOPHER MASAHI/JACKSON ROBART KABARA | NYUMBA MBILI | MTAA WA UTEMANI KATA YA MKOLANI PAMOJA NA NYUMBA ILIOPO MTAA WA KISEKE B KATA YA KISEKE MWANZA | 27/02/2021 |
| iv. | WANGWE INVESTMENT | WANGWE INVESTMENT | TWO PLOTS | MTAA WA SUSUNI KATA YA MAHINA (BUGARIKA)MWANZA | 02/3/2021 |
| v. | CECILIA M. MWAKISEKE MSIMAMIZI WAMIRATHI YA WILSON ULINDULA ANANGISYE | NYUMBA YENYE HATI NO. 18656-MBYL PLOT NA.2465, BLOCK NA.Y | NYUMBA | SAI -MWAKIBETE MBEYA MJINI | 24/02/2021 |

**MASHARTI YA MNADA**

Dhamana zitauzwa mahali zilipo

i. Mshindi atatakiwa kulipa asilimia ishirini na tano (25%) ya kiasi alichoshinda mara tu dalali atakapomtangaza kuwa mshindi (nyundo itakaposhushwa). Na 75% ndani ya siku 14.
ii. Gharama zozote ikiwemo za kubadilisha taarifa za nyaraka za umiliki ni za mnunuzi.
iii. Mshindi ataruhusiwa kuchukuwa Nyumba au kifaa/vifaa alivyonunua mara tu baada ya kufanya malipo kamili.

**Kwa mawasiliano zaidi**
**Simu ya dalali muhusika: 0713 077474 /0674 755313/0658370615**

HABARI KITAIFA

# Watalii waongezeka Hifadhi ya Burigi

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

IDADI ya watalii walioitembelea Hifadhi mpya ya Taifa ya Burigi inatia 'matumaini' katika uchangiaji wa pato la taifa, baada ya kuingiza kiasi cha Sh. 492,741, 622 hadi kufikia Desemba mwaka jana.

Bunge, limeelezwa kuwa jumla ya watalii 1,171 waliitembelea hifadhi hiyo, ambapo kati yao 996 ni wa ndani na 175 ni wa nje.

Waziri wa Katiba na Sheria, Mwigulu Nchemba, akiwasilisha bungeni juzi mapendekezo ya mpango wa tatu wa maendeleo wa taifa wa miaka mitano 2021/22-2025/26, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, alisema hifadhi hiyo imekusanya jumla ya Sh. 492, 741, 622 kati ya Novemba 2019 hadi Desemba mwaka 2020.

Wakati Hifadhi ya Taifa ya Nyerere, imetembelewa katika kipindi kama hicho na watalii 9,938, kati yao watalii 6,189 ni wa nje na watalii 3,749 ni wa ndani.

Katika hifadhi hiyo ya Nyerere, jumla ya Sh. 1, 552, 712, 660 zimekusanywa.

Waziri Mwigulu alisema: "Hatua hizo zimechangia kuongezeka kwa idadi ya watalii waliongia nchini kutoka watalii 1,137,182 mwaka 2015 hadi 1,527,230 mwaka 2019.

Aidha, wastani wa idadi ya siku zinazotumiwa na watalii kukaa nchini, zimeongezeka kufikia siku 13 mwaka 2019, ikilinganishwa na siku 10 mwaka 2015."

Kwa mujibu wa hotuba ya Waziri Mwigulu, mapato yatokanayo na utalii yameongezeka kutoka dola za Marekani bilioni 1.9 (sawa na Sh. bilioni 4,436.7) mwaka 2015, hadi dola za Marekani bilioni 2.6 (sawa na Sh. bilioni 6,071.3) mwaka 2019.

Katika kipindi cha serikali ya awamu ya tano, kiasi cha Sh. bilioni 269.7 kimetumika kuboresha na kuendeleza sekta ya maliasili na utalii.

# Tigo kuwapa wateja dakika 10 bure kila siku

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya simu za mkononi ya Tigo, leo inayo furaha kutambulisha huduma mpya ya Amka na Tigo.

Huduma hii itakua ikimpa fursa mteja wa Tigo kupiga simu bure katika mipango yake ya kila siku asubuhi.

Kila mteja wa Tigo atakuwa akipokea dakika 10 za bure kupiga simu za Tigo kwenda Tigo kuanzia saa 12:00 asubuhi hadi saa 3:00 asubuhi.

Hii ni ofa maalumu kwa wateja wa Tigo kwa ajili ya kuhakikisha wanakamilisha mipango yao pamoja na wapendwa wao.

Akizungumza Dar es Salaam, Meneja Mawasiliano kutoka Tigo, Woinde Shisael, alisema: "Tunataka kurudisha kwa wateja wetu ambao tumekuwa nao kwa kipindi chote kile tunachokipata.

"Tunaamini kila mteja wetu ni muhimu kwetu, ofa hii itasaidia kuimarisha mawasiliano baina ya wateja wetu na familia zao, marafiki na wanaofanya nao biashara kila siku asubuhi na mapema.

"Tigo ni chapa ambayo inaelewa mahitaji ya wateja wake na tunaamini Amka na Tigo itasaidia kila mteja wa Tigo kufanya mawasiliano kwa uhakika," alisema Shisael.

Tigo daima imekuwa ya kwanza kuuza na kutoa suluhisho za ubunifu zinazoleta mabadiliko mazuri sokoni.

Alisema Amka na Tigo itawezesha wateja wote wa Tigo, kwani watu wengi hupanga siku yao asubuhi kwa kuzungumza na familia, marafiki na wafanyabiashara.




Meneja Mawasiliano wa Tigo, Woinde Shisael, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati akitambulisha huduma mpya ya Amka na Tigo, itakayomwezesha mteja kupata dakika 10 za kupiga bure kila siku kuanzia saa 12 asubuhi hadi saa tatu asubuhi. Kushoto ni Meneja wa Kitengo cha Biashara wa kampuni hiyo, Ndevonaeli Eliakimu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wakuu wa shule wapewa meno kuwadhibiti walimu

**Na Richard Makore,** MWANZA

SERIKALI imewataka walimu wakuu wa shule za msingi kusimamia ubora wa elimu katika shule zao ikiwamo kudhibiti walimu wasiofanya maandalizi kabla ya kuingia katika vipindi pamoja na wale wanaochati darasani badala ya kufundisha.

Hayo yalisema jijini Mwanza na Mdhibiti Mkuu Ubora Shule za Msingi Kanda ya Magharibi, Felician Mwijage, wakati akifungua mafunzo ya siku tatu kwa walimu wakuu wa shule za msingi Mkoa wa Geita.

Mwijage alisema ubora wa elimu unaanzia kwenye maandalizi ya walimu kabla ya kuingia darasani na namna walivyojipanga kufundisha wanapokuwa darasani.

Aliwataka walimu wakuu kufuatilia ubora wa elimu katika shule zao ikiwamo kujua kinachofundishwa kama kinaendana mitaala iliyopo.

Aliwataka kutumia mafunzo hayo ya siku tatu kwa walimu wakuu na maofisa elimu wa wilaya, kudhibiti ubora wa elimu katika maeneo yao.

Meneja wa Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM), Kanda ya Mwanza, Venant Fundi, alisema, jumla ya walimu wakuu 16,300 watapatiwa mafunzo hayo nchi nzima.

Alisema mafunzo ya udhibiti ubora wa elimu ni muhimu kwa kuwa yanaongeza ufaulu kwa shule husika pamoja na kusaidia kupata ujuzi wa uongozi na utawala.

Aliongeza kuwa awamu ya kwanza inayoendelea watatoa mafunzo kwa walimu 8,000 na kwamba walimu wengine 8,300 watafundishwa awamu ya pili.

Mmoja wa walimu waliopatiwa mafunzo kutoka Shule ya Msingi Kanyala wilayani Geita, Regina Chrisostom, alisema moja ya changamoto wanazopata katika ufundishaji ni pamoja na darasa kuwa na idadi kubwa ya wanafunzi.

# Watendaji wasiotumia ilani ya CCM kukiona

**Na Anthony Gervas,** MAGU

WILAYA ya Magu mkoani Mwanza, imewaonya watendaji na viongozi wazembe watakaoshindwa kutumia ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), yenye kurasa 303, kutekeleza miradi ya maendeleo ya wananchi watatumbuliwa.

Angalizo hilo lilitolewa na Mkuu wa Wilaya hiyo, Salum Kali kwenye Baraza la Madiwani na watendaji wa idara mbalimbali katika Halmashauri ya Wilaya hiyo.

"Ilani ya sasa itawaumiza wengi watendaji na viongozi wazembe, tumieni ilani hiyo kujua miradi iliyokusudiwa na serikali kutekelezwa, vinginevyo mtakaa pembeni, nasema kweli daima kurudi nyuma kwangu mwiko, kila mtu atashika msara wake mwenyewe, alisema.

HABARI BUNGENI

# Mkopo kuineemesha Tarime maji

SERIKALI imepata mkopo kutoka serikali ya India kupitia Benki ya Exim India wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 500 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji katika miji 28 ya Tanzania Bara.

Moja ya miji itakayonufaika na mkopo huo ni pamoja na Tarime ambao utatumia chanzo cha Ziwa Victoria.

Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Esther Matiko, aliyetaka kujua lini mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria kwenda Tarime utakamilika.

Mahundi alisema kwa sasa mradi uko katika hatua za ununuzi wa makandarasi wanaotarajiwa kuwapo eneo la mradi ifikapo Aprili, mwaka huu, na ujenzi wa miradi unatarajiwa kuchukua miezi 24.

Awali, alisema wananchi wa mji mdogo wa Tarime wanapata huduma ya maji safi na salama kupitia mradi wa maji wa mserereko wa Nyandulumo, visima vitatu vya Rebu, Jeshi la Wokovu na Viambwi na bwawa la maji Tangota.

Kwa mujibu wa Mahundi, vyanzo hivyo vyote vinazalisha wastani wa lita 1,200 kwa siku wakati jumla ya mahitaji ni lita 6,000 za maji kwa siku.

"Utekelezaji wa mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria utahudumia maeneo yote ya mji wa Tarime kwa kuzalisha wastani wa lita 6,500 kwa siku ambazo ni zaidi ya mahitaji," alisema.




Habari na Augusta Njoji



Mbunge wa Kinondoni, Tarimba Abbas (kulia), akijadiliana jambo na Mbunge wa Mtama, Nape Mnauye, Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Kaya maskini zafikiwa halmashauri 39

BUNGE limeelezwa kuwa tayari serikali imeshaanzisha kanzidata ya walengwa wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini Awamu ya Tatu na tayati halmashauri 39 zimefikiwa.

Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deogratius Ndejembi, aliyasema hayo jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Neema Lugangira.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji serikali ina mpango gani wa kuanzisha kanzidata kwa kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) kuhakikisha wanaonufaika ni wale wanaokidhi vigezo vilivyowekwa na kuondoa mianya ya watu wanaonufaika kupata mara mbili kwenye maeneo tofauti.

"Serikali ina mpango gani kuhakikisha kaya ambazo hazijanufaika awali sasa zitanufaika katika awamu hii ya tatu hususan wazee?" Alihoji.

Akijibu maswali hayo, Ndejembi alisema awali utaratibu huo ulianza kwa halmashauri 19, lakini hadi sasa halmashauri 39 zimefikiwa na tayari wameanza kuweka mfumo wa kuunganisha na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) na mitandao ya simu.

"Ili walengwa badala ya kupokea fedha dirishani ziende moja kwa moja kwenye simu na kusiwe na malalamiko ya malipo mara mbili kwa walengwa na lengo ni kufikia halmashauri zote nchini," alisema.

Ndejembi alimhakikishia mbunge huyo kuwa kaya ambazo zina sifa ya kupata fedha hizo zinazotolewa kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) na hazikupata fursa hiyo kwenye awamu ya pili, zitaanza kunufaika kwenye awamu ya tatu.

"Mpango huu unaenda kwenye kaya milioni 1.4 sawa na watu milioni saba wanaenda kunufaika na mpango huu wa TASAF," alisema.

Katika swali la msingi, mbunge huyo alisema kumekuwapo na malalamiko kutoka kwa wananchi wa Manispaa ya Bukoba kuwa wanufaika wa TASAF ni wananchi wenye uwezo badala ya kaya maskini.

"Je, hayo ndiyo malengo ya kuanzishwa kwa TASAF?" Alihoji.

Naibu Waziri Ndejembi alisema malengo ya TASAF ni kuzinusuru kaya maskini katika halmashauri zote za Tanzania Bara, Unguja na Pemba kwa upande wa Zanzibar.

"Awamu ya kwanza ilianza rasmi mwaka 2000 hadi 2005, awamu ya pili ilianza mwaka 2005 hadi 2012 na awamu ya tatu kipindi cha kwanza ilianza kutekelezwa mwaka 2013 hadi Desemba, 2019 na kipindi cha pili cha awamu ya tatu kilianza Februari 2020 hadi 2023. Jumla ya kaya maskini milioni 1.1 zimeandikishwa na wanufaika kunyanyua hali yao ya kimaisha," alisema.

# Watumia mitumbwi kisa barabara mbovu

MBUNGE wa Malinyi (CCM), Antipas Mgungusi, amesema wananchi wake wa Kijiji cha Misegese wanalazimika kutumia mitumbwi kufika Malinyi mjini kutokana na barabara kutopitika wakati wote na hasa msimu wa mvua.

Kutokana na hali hiyo, ameiomba serikali kulitafutia ufumbuzi ikiwamo kuongeza idadi ya makalavati yatakayochepusha maji.

Akiuliza maswali bungeni jana, Mgungusi alisema sehemu ya barabara ya Lupiro, Malinyi, Londo hadi Namtumbo, yenye urefu wa kilometa 296 katika Kijiji cha Misegese kufika Malinyi mjini haifikiki kipindi chote.

"Hata mvua ikinyesha siku moja tunalazimika kutumia mitumbwi kufika Malinyi mjini na magari hayafiki kabisa. Mkandarasi aliyepo anaweka kalavati moja badala ya sita au saba yanayotakiwa amepewa kazi ya kuinua tuta kwa mita 200 badala ya kilometa moja," alisema.

"Je, serikali haioni kuna haja ya kumwongezea uwezo kulingana na uhitaji, pia Waziri yupo tayari kuongozana na mimi kwenda Malinyi kujionea hali halisi ya miundombinu na kutafuta suluhisho la pamoja?" Alihoji.

Katika swali la msingi, mbunge huyo alihoji ni lini serikali itaanza ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara hiyo ambayo ipo katika Ilani ya CCM 2020.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Godfrey Kasekenya, alisema barabara hiyo imekuwa ikiuliziwa na wabunge wanufaika wa barabara hiyo na atafanya ziara ili kufanya utatuzi.

"Kuhusu mkandarasi tutaongea na Meneja wa Wakala wa Barabara (TANROADS) ili kuangalia tatizo lililopo na afanye kulingana na matakwa yaliyopangwa," alisema.

Katika majibu ya swali la msingi, Naibu Waziri huyo alisema barabara hiyo ni sehemu ya barabara kuu ya Mikumi - Kidatu - Ifakara - Malinyi - Kilosa kwa Mpepo - Londo - Lumecha yenye jumla ya kilometa 547 ambayo inaunganisha mikoa ya Morogoro na Ruvuma.

Alisema serikali kwa kuzingatia umuhimu wa barabara hiyo Wizara kupitia TANROAD imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina mwaka 2018.

## Viongozi wa Afrika miaka 60 madarakani bado bara liko hoi

Ukurasa 13





Ukurasa 14

## India inavyojituma kutekeleza malengo ya Paris

siasa

JUMATANO FEBRUARI 10, 2021

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe

UCHAMBUZI

# Lipumba na pakuanzia kuelekea Katiba mpya



Prof. Lipumba akichangia mijadala ya Bunge Maalumu la Katiba lililofanyika Dodoma mwaka 2014. **PICHA MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI wa CUF, Profesa Ibrahim Lipumba, hivi karibuni 'ameliamsha dude' akimwomba Rais John Magufuli, kukumbuka zawadi muhimu Watanzania wanayoingojea kwa muda mrefu ya kuwapo kwa katiba mpya.

Katiba ndiyo msingi unaowapa watawala uhalali wa kuwaongoza wananchi, baada ya umma kukubaliana mambo yote ya msingi na yanayohitajika kudumishwa na kulindwa kisheria na kikatiba, na ndicho chombo pekee kinachosimamia haki, amani, utii wa sheria na heshima kwa wale inayowasimamia.

Itakumbukwa kuwa miaka sita imepita sasa baada ya kuundwa Bunge Maalum la Katibu lililoanza kazi baada ya Tume ya Jaji Warioba, kukusanya maoni na mapendekezo ya kuundwa katiba mpya.

Bunge maalumu liliichambua rasimu ya katiba mpya, iliyoandaliwa na Tume ya Warioba, lakini lilishindwa kuwapa Watanzania katiba waliyoitamani, ndiyo maana Lipumba anamkumbusha Rais Magufuli, kuwapatia Watanzania kile wanachotaka au katiba mpya, ambayo wameitamani kwa miaka mingi.

Anamkumbushia kuhusu kuyaangalia tena maoni ya wananchi yaliyotoa rasimu ya katiba ambayo Bunge Maalumu liliyafanyia uchambuzi, lakini halikufanikisha kupatikana andiko hilo.

Analosema Profesa Lipumba ni jambo jema kwani Tanzania inahitaji katiba inayoandaliwa inayokuwa na muafaka na maridhiano ya kitaifa na inayotengenezwa kwa ridhaa ya wadau wote au walio wengi na inayokubalika na raia wengi.

Ni kama Profesa Lipumba anazungumza kile ambacho kipo kwenye mawazo ya wanasiasa wengi, wanazuoni, wadau wa uchaguzi, taasisi za kirai na Watanzania ambao wanaona kuwa ni wakati wa kuandika na kuwa na sheria kuu ambayo inakubalika na wengi.

Licha ya kwamba wakati wa maandalizi ya katiba mpya yaliyofanywa na Bunge la Katiba, Lipumba aliunda Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA) uliounda na vyama vya siasa kwa lengo la kutetea maoni ya wananchi baada ya kuhisi pengine mambo yatakwenda ndivyo sivyo, ama kuwa wa kwanza kueleza azma ya katiba mpya mbele ya Rais.

Lakini, si UKAWA pekee hata baadhi ya viongozi wa dini hawakukubaliana na mwenendo ulivyokuwa nao pamoja na baadhi ya vyama vya kirai, wajumbe hao walikuwa wakiunga mkono UKAWA.

UKAWA, Tume ya Warioba ya Kuratibu Maoni ya Katiba Mpya, baadhi ya wasomi na hata wananchi mmoja mmoja waliona kuwa katiba pendekezwa huenda ilikosa uhalali wa kitaifa kwa kukosa maridhiano.

Kama anavyosema Profesa Lipumba pengine huu ndiyo wakati wa kukaa pamoja wadau wote muhimu kukubaliana cha kufanya na hasa kuipa mwafakwa wa kitaifa.

Kwa sababu katiba iko juu ya yeyote, inatakiwa isifungamane na chama tawala, dola wala viongozi. Ni sheria kuu na lazima iandaliwe na kuandikwa kwa kuridhiana kwa vile ndicho kiongozi cha viongozi wa taifa.

Kama Profesa Lipumba anavyoshauri ni vyema serikali kuona umuhimu wa kukutanisha wadau muhimu kuanzia wanasiasa, wanahabari, viongozi wa dini, wasomi, wataalamu wa sheria, wachumi, sekta binafsi, asasi za kiraia, mahakama, polisi, wanasiasa wastafu na hata wataalamu kutoka nje ya nchi kuamua jambo jema la kufanya na wapi pa kuanzia ili kuwa na katiba mpya yenye ridhaa ya kitaifa na kukubaliwa na wananchi.

Kazi iliyofanywa na Tume ya Warioba inatosha hivyo, pengine hakuna sababu ya kuongeza gharama kubwa zaidi kwa walipa kodi wa Tanzania kwa kuanzisha tena safari ya kwenda kwa wananchi kwa kuunda tume nyingine ya kukusanya maoni.

Hata hivyo ni vyema bunge likashauriana na serikali kwani wao ndiyo wawakilishi wa wananchi ili kufahamu namna bora ya kupata katiba mpya.

**TUME YA KITAALAMU**

Moja ya mambo ambayo serikali na wadau hasa wawakilishi wa wananchi wanaweza kufikiria ni kuunda Kamati ya Kitaalamu itakayochambua rasimu ya Warioba na ya Bunge au katiba pendekezwa.

Kwa kutumia utaratibu wa kukubaliana ama kutokukubaliana wajumbe hao wa tume ya kitaalamu watapata muafaka wa katiba ambayo itabeba maudhui ya kuridhiana.

Hiyo ndiyo kama wadau wakikubaliana ifikishwe bungeni na kujadiliwa ili kuongezewa mambo muhimu zaidi, lakini si kufumuliwa kama ilivyofanywa na Bunge Maalumu la Katiba 2014.

Taarifa za kimtandao, zinaonyesha kuwa baada ya Kenya kukwama kupata katiba mpya ilibidi kuunda Tume ya Kitaalamu iliyokuwa na wabobezi wa masuala ya katiba waliotoka nje na ndani ya Kenya.

Mtandao unaeleza kuwa wabobezi waliofanikisha kuziweka pamoja rasimu mbili za katiba

INAENDELEA UK. 12



Mamia ya Wasomali wakiwa kambini kutokana na ukosefu wa amani katika taifa hilo. **PICHA: MTANDAO**

# Viongozi wa Afrika miaka 60 madarakani bado bara liko hoi

**Na Nimi Mweta**

NCHI za Afrika takribani zote zimefikia miaka 60 ya uhuru, lakini bado swali ambalo wachambuzi walilokuwa wanajiuliza tangu 1960 baada ya kupata uhuru kutoka kwa wakoloni wakongwe, limebakia pale pale. Ni hii Afrika inayojitawala itaweza kulinda amani au kila siku inaendelea kuomba msaada nje?

Kinachoulizwa hapo si kuomba misaada ya maendeleo kwani hata miongoni mwa nchi zilizopiga hatua kimaendeleo suala hilo lipo, cha msingi ni uwezo wa kuishi kama taifa lenye dhamira ya pamoja na taratibu ambazo jamii hiyo inajiwekea ili nchi iendeshwe kwa utaratibu unaoeleweka siyo kila mara makundi ya watu, raia na wale wenye silaha kula njama kuvuruga serikali.

Kinachoshangaza zaidi ni kuwa Afrika haijui kuwa inalo tatizo. Hata leo ni nchi chache ambazo haziko katika vita moja au nyingine. Inaweza kuwa kujitenga, kupindua serikali, au makundi yenye silaha kuundwa ili kuwanyang'anya wananchi mifugo na ardhi.

Wapo wanaoachwa katika makambi ya wakimbizi kwa miongo kadhaa bila matumaini ya kurudi, au baada ya miaka 20 serikali ikibadilishwa.

Unapata picha ya kinachotokea ukisikiliza vyombo vya habari kwa mfano kuhusu mkasa wa kutokuwapo serikali nchini Somalia, kwa kushindwa kuafikiana kupata kiongozi mpya, au Libya hivi karibuni kufikishwa mezani na kupatikana kiongozi wa mpito (waziri mkuu) na 'wajumbe watatu wa 'kamati ya urais' wanaopokezana uenyekiti wakati wa kipindi cha mpito. Mchambuzi mmoja wa Chuo Kikuu cha Tumaini akizungumzia suala la Somalia anasema tatizo nchini humo ni kutotenda haki, kwa kuwa viongozi wanashindana wao kwa wao nani awe mkuu, au mjumbe lakini watu hawashirikishwi.

Anasisitiza kuwa suala la haki limalizwe kwanza, wakati siyo rahisi kusema ni haki gani inazungumziwa hapo, wakati hakuna utawala nchini humo. Kujadili nia ya kutanguliza haki ni kutetea haki ya watu wa Somalia kujichagulia au kutawaliwa na serikali inayotokana na wao wenyewe bila kuingiliwa na nchi za nje. Kwa mustakabali huo, ni wazi Al Shabaab itashinda Somalia na kuendeleza moto wake maeneo yaliyobaki ukanda wa mashariki wa Afrika na Taliban huko Afghanistan.

> Wapo ambao wamekuwa wakisema kinachosemwa kuhusu Afrika kuwa 'shimo la choo' kama alivyosema aliyekuwa Rais wa Marekani, Donald Trump, mwanzoni mwa utawala wake 2017 ni aina ya ubaguzi.

Jambo la msingi hapa ni kukwama kwa kile kinachoitwa maendeleo kwa maana ya mabadiliko makubwa katika mifumo ya maisha ya jamii. Ni nadharia inayofundishwa vyuoni ambayo inaweka ngazi kadhaa za nchi kupitia katika maendeleo yake, hasa kuacha uchumi wa kilimo kuingia wa viwanda, kuacha maisha ya vijijini na kuanzisha ya mijini kuacha imani za kizamani za jadi au za dini ili kujenga nchi yenye misingi yake katika sheria inayoridhiwa na raia kupitia Bunge.

Wapo ambao wamekuwa wakisema kinachosemwa kuhusu Afrika kuwa 'shimo la choo' kama alivyosema aliyekuwa Rais wa Marekani, Donald Trump, mwanzoni mwa utawala wake 2017 ni aina ya ubaguzi.

Kilichotokea nchini Marekani, ambako rais huyo alihutubia kundi la wafuasi wake akiwahamasisha wateke makao makuu ya serikali na mabaraza ya bunge la nchi hiyo (Congress) ili kuzuiwa 'kuibwa' uchaguzi mkuu, ingekuwa ni Afrika nchi ambaye ingefanya hayo ingesambaratika.

Kwa Marekani haikuwa hivyo, dhoruba hiyo ilipita kama vile nchi imepiga chafya na kanuni zikafuatwa kumalizia 'kiporo' cha kuthibitisha matokeo ya uchaguzi mkuu. Suala ni kuwa hawana ujadi wowote ila utawala wa sheria na katiba wakati Afrika inalilia jadi.

Kwa Afrika, matazamio kuwa maendeleo yangeleta mabadiliko ya teknolojia ambako maisha ya viwanda na mijini yangemaliza tatizo la ujadi sasa yamedidimia kwani teknolojia inaondoa kazi badala ya kuziongeza, nje ya zile za huduma kama 'vibanda umiza' vya kuangalia luninga zenye picha za ngono na kupeleka fedha kwa simu. Ina maana kuwa Afrika itaendelea kuwa na mamia ya maelfu ya vijiji katika karne hii na hivyo suala ni kumaliza ujadi katika akili za Waafrika na si kutazamia maendeleo makubwa ya viwanda. Ni pale makabila yakiishia mijini na kupoteza lugha zao, tunguri zao, makaburi ya babu zao na matambiko pia.

Afrika imeshindwa kukabiliana na ujadi huu kwa sababu haitaki wahamiaji wenye fedha kutoka nje, ikiwa ni pamoja na raia wa nchi hiyo waliohamia nje (kwa mfano kwenda kusoma na kubaki huko) kuja kununua mali isiyohamishika ili fedha zao ziongezeke thamani kwa kuwekeza katika ardhi. Ndiyo njia pekee ya kuhakikisha fedha inaongezeka thamani katika muda mrefu bila kuingia katika mpangilio wa kufuatilia thamani za hisa katika masoko ya fedha.

Waafrika hawawezi kuinua mitaji ya ndani kununua maeneo ya vijiji kwa thamani inayotakiwa, waliopo wahamie maeneo karibu na miji waanzishe biashara zenye uhakika na kuajiri watu, hivyo ununuzi huo upo ila ni kwa mwendo wa konokono; taabu.

Unaweza kusema kuwa hali ya uchumi duniani inayotokana na janga la corona, linavyoanza kudhibitiwa kuna athari zake katika uchumi kwa jumla. Hasa ni kupukutika kwa kazi nyingi, mazoea ya kufanya kazi nyumbani kuanza kushamiri na roboti kutumiwa zaidi viwandani na magari yanayojiendesha kuanza kutengenezwa.

Ni mazingira ambayo uwekezaji unaanza kupungua na hivyo fedha zitaanza kutafuta wapi kunafaa zipelekwe, na siyo tena China kwani mishahara inapanda halafu demokrasia imekwama.

Jitihada ya serikali ya sasa Marekani kuongeza kima cha chini kutoka dola tano za sasa hadi dola 15 kwa saa zitaongeza msukumo kufutafuta maskani mapya kuwekeza. Pengine itatoa mwanya wawekezaji wasinunue vijiji taratibu ili utamaduni ujifie, Afrika iondokane na janga la jamii ya wauaji, warithi ardhi iwe kwa mkuki, panga, risasi kupora ng'ombe au madini.

# Lipumba na pakuanzia kuelekea Katiba mpya

**INATOKA UK. 11**

ya Bomas na ile ya Wako walitoka Zimbabwe. Ukweli ni kwamba baadhi ya kanuni za kupata katiba zinadokeza kuwa si rahisi kuwa na katiba inayokubalika na wote kwa ulaini au urahisi.

Kwa maana hiyo ni lazima kutoka jasho na hata ikibidi kukabiliwa na chuki za kikabila na za kibaguzi na mataifa mengi kama Kenya na Afrika Kusini yanaweza kuwa mfano.

Mathalani, waliopata katiba bora baada ya chuki, ubaguzi na unyanyasaji uliopindukia ni Afrika ya Kusini. Kadhalika Ethiopia iliandika katiba bora baada ya vita vya miaka 27 na jirani yake Eritrea.

NJIA IMENYOOKA

Kwa Tanzania hilo si suala la kuhofisha kwa sababu serikali ilishaazimia kuwapo wananchi katiba mpya. Alichofanya Rais mstaafu Jakaya Kikwete ni kujibu kilio cha wadau wengi wakiwamo wanasiasa waliokuwa wanataka kuwapo na Tume Huru ya Uchaguzi, kubadilisha sheria za uchaguzi, kuboresha Muungano na kuongeza uwajibikaji.

Katiba ni mchakato unaoshirikisha wadau wengi na jambo muhimu kwa Tanzania ni kuwa na utaratibu wa kusikilizana, unaokubalika na wengi na wenye muafaka wa kitaifa ili kupata chombo hicho.

Wadau wa katiba ni pamoja na wananchi (raia) vyama vya siasa, wanahabari, asasi za kiraia, wanasiasa wenyewe, wanasheria, NEC, Mahakama, Wizara ya Sheria, Bunge, Polisi, Jumuiya ya Kimataifa pamoja na wadau wengine wa kimataifa ukiwamo Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika.

Kwa hiyo, katiba msingi wake lazima uwe ni maridhiano na kufanikisha mchakato huo kwa amani, ni vyema Bunge na Baraza la Wawakilishi vinavyohusika na mchakato wote wa kisheria na taratibu za kisheria za kupata katiba kuliangalia kwa jicho pevu jambo la maridhiano, muafaka wa kitaifa na maslahi ya taifa katika kupata katiba mpya.




Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally (wa tatu kulia) akiwa kwenye moja ya kampeni za chama hicho. **PICHA: MTANDAO**

## CCM MIAKA 44

# Mkongwe anayeendelea kuwaburuza wapinzani

**Na Sabato Kasika**

HISTORIA inavihukumu baadhi ya vyama vikongwe vilivyoleta ukombozi barani Afrika kuwa vimesambaratika baada ya kuingia kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa, vikiwamo KANU ya Kenya na Parmehutu ya Rwanda.

Vingine ni MNC cha Congo RDC, UNIP cha Zambia kilichoongozwa na Kenneth Kaunda, ambacho kilikuwa cha kwanza kuangushwa mwaka 1991 baada ya kukaa madarakani kwa miaka 27 katika uchaguzi mkuu uliompa Frederick Chiliba wa Chama cha MMD uongozi wa nchi.

Wakati vyama hivyo vikisambaratika, kwa Tanzania imekuwa ni tofauti, kutokana na chama kikongwe cha CCM, kuendelea kuimarika na kuwapo madarakani kwa miaka mingi tangu kilipoanzishwa 1977, Februari 5, mwaka huu, CCM imetimiza miaka 44 ikizaliwa baada ya kuunganishwa vyama ukombozi vya TANU na ASP.

CCM iliadhimisha miaka hiyo 44 kikiwa ni miongoni mwa vyama vichache na vikongwe vya ukombozi barani Afrika ambavyo hadi sasa vimeendelea kubaki madarakani na mwaka jana kilishinda kwenye uchaguzi mkuu uliofanyika Oktoba 28 kwa kupata asilimia zaidi ya 90 kwenye kura zote za udiwani, ubunge na urais.

Chama kimekuwa madarakani tangu ya enzi ya mfumo wa chama kimoja na kimeendelea kuongoza ndani ya mfumo wa vyama vingi, tangu uchaguzi wa kwanza ndani ya mfumo huo, uliofanyika mwaka 1995.

Kimsingi CCM haikuwapo wakati wa uhuru wa Tanganyika mwaka 1961 wala Mapinduzi ya Zanzibar 1964, lakini inaweza kuhesabika kama chama cha ukombozi kwa sababu kilizaliwa na vyama vilivyofanya kazi hiyo.

**SIRI YA MAFANIKIO**

CCM inaonekana kuwa bado ni maarufu katika baadhi ya jamii na inadumu madarakani, ingawa ndani ya miaka 29 ya mfumo wa vyama vingi vya siasa nchini imekabiliana na wimbi la upinzani hata baadhi ya majimbo kuwa mtihani mgumu kuyamiliki.

Hata hivyo, uchaguzi mkuu wa mwaka uliopita, chama hicho kimefanikiwa kutwaa majimbo mengi na ngome kongwe za upinzani hali inayoonyesha kuwa kimejijenga zaidi kwa wananchi na kuendelea kuungwa mkono.

Zipo sababu nyingi za kinazoelezea kwa nini CCM imeendelea kuwapo madarakani wakati vyama vingine vikongwe vikiwa vimeshafutika kwenye ulimwengu wa siasa au kubaki vikisuasua.

Miongoni mwake ni uimara, unaotokana na Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, kuijenga na kuliunganisha taifa kupitia chama hicho hivyo kuwa miongoni mwa siri ambazo zinaelezwa kuifanya CCM kuendelea kuaminiwa na wananchi, kutokana na kusimamia amani na utulivu wa taifa.

Kutokana na heshima ya chama iliyojengwa na mwenyekiti wa kwanza wa chama hicho, wananchi wanaiona CCM kama urithi wa Nyerere, hivyo kuondoka katika chama hicho ni kama kusaliti.

> Mambo kama hayo yawe ni darasa kwa CCM na kuhakikisha kero zote zinazowakabili Watanzania, zinapatiwa ufumbuzi, lakini viongozi wakibweteka na kuona ni jambo la kawaida, yaliyovikuta vyama vingine vikongwe yanaweza kutua katika chama hicho.

Kukaa madarakani kwa miaka mingi, kusiwafanye viongozi wa CCM kubweteka na kudhani kuwa vyama vikongwe haviwezi kuondoka madarakani, bali lolote linaweza kutokea.

Inawezekana, Watanzania wanavitumia vyama vya upinzani kama mahali pa kuonyesha hasira zao pale serikali na CCM wanaposhindwa kukidhi matarajio yao katika kusimamia mambo muhimu ya nchi.

Mambo kama hayo yawe ni darasa kwa CCM na kuhakikisha kero zote zinazowakabili Watanzania, zinapatiwa ufumbuzi, lakini viongozi wakibweteka na kuona ni jambo la kawaida, yaliyovikuta vyama vingine vikongwe yanaweza kutua katika chama hicho.

**MIKAKATI YA SASA**

Kwa mujibu wa Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally, chama kina mikakati mbalimbali ya kujiimarisha ambayo itakifanya kiendelee kuaminiwa na Watanzania, ikiwamo kusimamia serikali ipasavyo.

"Vilevile tunafanya uhakiki wa kina kwa kusajili wanachama kielektroniki ili tuwe na taarifa za uhakika kwa sababu chama chetu ni kikubwa sana. Tuna matawi zaidi ya 24,000," anasema Dk. Bashiru.

Katibu mkuu huyo anasema, wanachama hao na wengine ambao wanaiamini CCM ndiyo walioipa ushindi wa kishindo kuanzia madiwani hadi wabunge na kwamba, ushindi huo una manufaa makubwa, kwani chama ni watu na kwamba katika matawi ndiko wanakopatikana wanachama, hivyo CCM itaendelea kujiimarisha kwenye ngazi hiyo kujihakikishia ushindi zaidi.

Mbali na hilo, Dk. Bashiru anasema, CCM ina mabalozi 250,000 nchini nzima, ambapo taarifa zao zimo kwenye mfumo wa kidijitali, na kwamba chama kinaendelea kufanya makubwa zaidi. Katibu mkuu huyo anasema, wanachama hao na wengine ambao wanaiamini CCM ndiyo walioipa ushindi wa kishindo kuanzia madiwani hadi wabunge na kwamba, ushindi huo una manufaa makubwa.

Anataja manufaa hayo kuwa ni madiwani na wabunge kusimamia mipango na kufikia malengo bila kuyumba, lakini pia anatoa angalizo kwa washindi hao kwamba, watakienda kinyume na maadili na uadilifu, CCM haitakaa kimya bali itawachukulia hatua ikiwamo kuwavua uanachama.

"Ninachotarajia ni kwamba, wingi huo wa madiwani na wabunge, chama na serikali watafanya kazi kwa pamoja, lakini hata hivyo chama hakitapoteza jukumu lake la kuisimamia serikali," anasema.

Jambo ambalo anawakumbusha ni kuwa kupitia vikao vya kata na baadaye mabaraza ya halmashauri, wilaya na manispaa na majiji, wataendelea kuisimamia serikali.

# India inavyojituma, kujiongeza kutekeleza malengo ya Paris

## •Kumaliza changamoto mabadiliko ya tabianchi

NA HARSH VARDHAN SHRINGLA

MIAKA mitano baada ya Azimio la Paris linalohusu kupunguza kwa kiasi kikubwa uzalishaji wa hewa ya ukaa pamoja na ongezeko la joto duniani, India ni miongoni mwa nchi chache zinazoendelea ambazo si tu zinafikia malengo yake ya 'kijani kibichi' bali pia zinakusudia kuwa na mipango mikubwa zaidi kuhusiana na mabadiliko ya tabianchi.

Azimio au Mkataba wa Paris wa mwaka 2015 ni makubaliano ya mataifa mbalimbali ya kuweka nguvu za pamoja kudhibiti ongezeko la joto duniani juu ya nyuzi joto 2.0 na kujitahidi kulishusha hadi nyuzi 1.5 ikiwa ni jitihada za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Katika mkutano kuhusu Malengo ya Tabianchi, Waziri Mkuu, Narendra Modi, anaelezea mbinu ya India kuhusiana na tabianchi. Anasema ni lazima tuyaweke matazamio yetu 'juu zaidi', bila kuyasahau malengo ya awali. Anaongeza kuwa si tu kwamba India itayafikia malengo ya Azimio la Paris, bali itayafikia, kuyatekeleza na kuyavuka.

Katika Mkutano wa Umoja wa Mataifa (UN), kuhusu hatua dhidi ya tabianchi mwaka 2019, Modi anasema kwamba, kitendo kidogo kina thamani kubwa zaidi kuliko tani moja ya maneno. Tunachukua hatua za kivitendo katika maeneo yote, ikiwamo nishati, viwanda, usafirishaji, kilimo na ulinzi wa maeneo yenye kijani kibichi, katika safari yetu yote ya kijamii kuelekea katika kuwa kinara wa vitendo na malengo kuhusiana na mabadiliko ya tabianchi.


Waziri Mkuu, Narendra Modi

India inatambua kwamba mabadiliko ya tabianchi hayawezi kushughulikiwa bila kutumia mbinu mseto (mchanganyiko), imara na ushirika wa pamoja. Mabadiliko haya ya tabianchi yanahitaji ubunifu na utumiaji wa teknolojia mpya na endelevu. Ikiwa inatambua umuhimu wa mambo haya, India imeliingiza suala la tabianchi katika mikakati yake ya kitaifa ya maendeleo na viwanda.

Nishati ndicho kitovu cha mikakati yote ya tabianchi. Tunaamini kuwa India imekuwa ni nchi yenye nishati safi au mbadala na ni kinara katika ubadilishaji wa nishati kutoka katika vyanzo vya nishati vinavyotoa hewa ya ukaa kwenda katika vyanzo vya nishati mbadala na vya mafuta visivyo vya asili.

Tunakusudia kuendelea kuvuna hazina ya nishati mbadala ya India. Uwezo wetu wa nishati mbadala ni wa nne kwa ukubwa duniani na uongezaji wa uwezo unaofanywa sasa ni miongoni mwa uongezaji uwezo mkubwa pia duniani. Sehemu kubwa ya nishati hii itatoka katika chanzo cha nishati safi zaidi, yaani jua.

Hata sasa tunaona kuna maendeleo kuhusiana na hili. Katika hatua za awali tulikusudia kuwa na uwezo wa kupata Giga Watts (GW) 175 ya nishati mbadala ifikapo 2022. Tumeenda mbali zaidi na kutarajia kuvuka kiasi cha GW 220 katika kipindi cha miaka miwili ijayo. Aidha, tuna malengo makubwa zaidi ya kuwa na GW 450 ifikapo 2030.

Tunapambana kuhakikisha kwamba asilimia 40 ya umeme nchini India itokane na vyanzo vya nishati isiyohusiana na mabaki (ya asili) ifikapo mwaka 2030. Shabaha hii ya kuwa na nishati safi inayokwenda sambamba na jitihada za kupunguza kiwango cha uzalishaji joto na hewa chafu katika uchumi wa taifa hili kwa asilimia 33 hadi 35 (kutoka viwango vya 2005) ifikapo mwaka 2030.

Mradi wa Ujala - mkakati wa kitaifa wa kutumia taa za LED unapunguza uzalishaji wa tani milioni 38.5 za carbon dioxide ($CO_2$) kila mwaka. Aidha, mradi wa Ujjwala, ambao kupitia huo zaidi ya kaya milioni 80 zimefikiwa na huduma ya gesi safi ya kupikia, ni mojawapo ya jitihada kubwa za uzalishaji nishati safi duniani.

Jitihada za kupambana na mabadiliko na uhifadhi wa tabianchi vimeingizwa katika mipango ya serikali katika sekta mbalimbali. Mpango wetu wa Majiji Bora unafanya kazi na majiji 100 ili kuyasaidia kuwa endelevu zaidi na yanayoendana na changamoto ya mabadiliko ya tabianchi.

Vilevile, Programu ya Kitaifa ya Hewa Safi inalenga kupunguza uchafuzi wa hewa kwa asilimia 20 hadi 30 katika kipindi cha miaka minne ijayo.

Mpango wa Jal Jeevan, unaolenga kutoa majisafi na salama ya kunywa ya kutosha kwa kuunganisha bomba katika kila kaya ifikapo 2024 kwa familia zote za India vijijini, nao una shabaha madhubuti na ya kudumu.

Miti mingi imepandwa na ardhi yenye mmomonyoko na iliyoharibika inarudishwa katika hali bora ili kutengeneza mazingira yanayoweza kufyonza tani bilioni 2.53 za hewa ukaa au kaboni ($CO_2$).

Vilevile, tunashughulika kwa kasi kutengeneza mtandao wa usafiri wa kijani (usiotegemea nishati asilia), kubadilisha sekta ya usafiri inayojulikana kwa uzalishaji wa hewa chafu hususan katika majiji yetu makubwa.

India inatengeneza miundombinu ya kizazi kipya kingine kama vile mifumo ya usafiri wa watu wengi, barabara rafiki kwa mazingira (barabara za kijani) na njia za majini. Mpango wa kitaifa wa magari ya umeme unatengeneza mfumo wa ikolojia wa magari-umeme ukiwa na lengo la kuwa na magari yanayotumia umeme zaidi ya asilimia 30 ya magari yote katika barabara za India.

Mikakati hii ni kwa ajili ya faida yetu wenyewe kwani India ni miongoni mwa nchi zinazoathiriwa sana na matokeo ya mabadiliko ya tabianchi.

Tunatambua kwamba bado kuna safari ndefu katika hili, lakini jitihada hizi tayari zimeanza kuzaa matunda. Kiwango cha uzalishaji wa hewa chafu nchini India kimepungua kwa asilimia 21 katika kipindi cha kuanzia mwaka 2005 hadi 2014. Katika muongo ujao, tunatarajia kwamba kitazidi kupungua zaidi.

India inalenga kuwa mwajibikaji wa kimataifa katika masuala ya tabianchi. Hatuvuki tu azma zetu za Azimio la Paris bali tunatumia pia zana za kiubunifu kuendeleza na kuukuza ushirikiano wa kimataifa katika hatua dhidi ya tabianchi.

Tumeanzisha mashirika ya kimataifa kama International Solar Alliance na Coalition for Disaster Resilient Infrastructure ambayo yanafanya kazi ya kuweka mbinu na mikakati ya kidunia katika kupunguza hewa ukaa (kaboni). Zaidi ya nchi 80 zimeungana na International Solar Alliance, na kulifanya kuwa miongoni mwa vyombo vya kimataifa vinavyokua kwa haraka.

Muunganiko huu wa hatua za kitaifa na kuwa raia wa kimataifa mwajibikaji huifanya India kuwa ya kipekee miongoni mwa nchi zinazoendelea na huiweka katika nafasi ya kuyaona malego yake kuwa kiongozi kifikra na kivitendo kuhusiana na tabianchi.

***Harsh Vardhan Shringla ni Katibu Mkuu wa Mambo ya Nje wa India. Mitazamo iliyoelezwa ni yake binafsi.***



## HABARI DODOMA

# Tahadhari yatolewa dhidi ya wanaodai kutibu COVID-19

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WATAALAMU wa tiba asili wamewataka Watanzania kuchukua tahadhari dhidi ya matapeli wa tiba hizo wanaojitokeza kuwa wao ni mabingwa wa kutibu ugonjwa wa COVID-19.

Wametoa hadhari hiyo kipindi hichi ambacho serikali inahimiza matumizi ya tiba hiyo.

Angalizo hilo lilitolewa na Said Mbogo, mtaalamu wa tiba ya asili wakati akizungumza na waandishi wa habari, kuhusiana na wimbi kubwa linaloweza kujitokeza la waganga wa kienyeji kudai kuwa na uwezo wa kutibu ugonjwa wa corona.

Mbogo alisema kuwa kutokana na waganga hao kuanza kuibuka kwa kipindi hiki ambacho serikali imetoa ruhusa ya kujifukiza, Watanzania wanapaswa kuwa waangalifu na matapeli hao wanaojifanya kuwa na uwezo wa kutibu corona.

Pia wamewataka waganga wa tiba asili kuhakikisha wanapata usajili ili watambulike kisheria na waaminiwe na serikali na wateja wanaowahudumia.

Naye mtaalamu wa tiba za asili, Benjamin Mzuri, ameiomba serikali kuanzisha kliniki ya tiba asili ili waweze kutambuliwa na kuwawezesha kuwasaidia Watanzania walio wengi.

Alisema kuwa kliniki hiyo itathibitisha dawa zinazotokana na mimea ya asili kwa mkemia mkuu na watumiaji kabla ya kuwahudumia wateja wao kwa ajili ya kuwalinda kiafya.

Aidha, amekiomba chama cha waganga wa tiba asili kuwasimamia waganga hao ili kupatiwa leseni ambayo itawawezesha kufanya kazi zao kwa uwazi na uhuru tofauti na ilivyo sasa, ambapo wengi wao wanahusishwa na utapeli.

# Mbunge achangia mil. 600/- ujenzi wa madarasa

**Na Ibrahim Joseph,** CHAMWINO

MBUNGE wa Chamwino, Deogratius Ndejembi, amechangia Sh. milioni 600, kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa ya Shule ya Sekondari Msamalo.

Aidha, amezitaka kamati za ujenzi za shule nchini kuhakikisha wanasimamia ujenzi wa majengo ya serikali kwenye maeneo yao.

Mchango huo wa fedha aliutoa juzi wakati alipokuwa akizungumza na viongozi wa vijiji na mitaa pamoja na viongozi wa madhehebu ya dini mbalimbali Kata ya Msamalo.

Ndejembi, alisema ametoa mchango huo kutokana na shule hiyo kukabiliwa na matatizo ya upungufu wa vyumba vya madarasa na utekelezaji huo ni sehemu ya ahadi yake aliyoitoa wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu 2020.

Alisema shule hiyo inahitaji kuendelezwa kwa kuwa ni pekee ya sekondari katika kata hiyo na inahudumia wananchi wengi kutoka kutoka kijiji jirani, hivyo inahitaji kuboreshwa ili kuinua kiwango cha elimu.

Pia alibainisha kuwa fedha hizo zitajenga vyumba vitatu vya madarasa pamoja na kununua samani zake ambazo ni viti na meza.

Kadhalika, alisema fedha hizo zitasaidia kujenga vyoo vya shule vitakavyotumiwa na wanafunzi kutokana na shule hiyo kuwa na upungufu mkubwa wa matundu ya vyoo.

Aidha, alizitaka kamati za ujenzi za shule nchini kuhakikisha wanasimamia ujenzi wa majengo ya serikali yanayojengwa kwenye maeneo yao na wajenge uaminifu kwa kuwasimamia mafundi na wale wanaonunua vifaa.

Hata hivyo, aliahidi kutembelea miradi hiyo kila mwisho wa wiki ili kuhakikisha inakamilika kwa wakati.

Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Msamalo, Allen Mmasa, alimshukuru mbunge huyo kutokana na kuwasaidia kuondoa tatizo la upungufu wa vyumba vya madarasa na matundu ya vyoo.

Alisema shule hiyo ina wanafunzi 6,019 na mwaka huu ilitakiwa kupokea wanafunzi 238 wa kidato cha kwanza, lakini kutokana na tatizo la vyumba vya madarasa wamepokea wanafunzi 100 pekee.

Aliongeza kuwa kutokana na mchango huo uliotolewa na Mbunge utasaidia kujenga vyumba ambavyo vitatosheleza idadi ya wanafunzi walioshindwa kujiunga na shule.

Pia alisema ujenzi huo wa vyumba vya madarasa utakapokamilika utasaidia kupunguza msongamano wa wanafunzi darasani na kuwawezesha walimu kufundisha vizuri.

Ofisa Elimu Wilaya ya Chamwino Sekondari, Rehema Nahale, alisema wilaya inakabiliwa na tatizo la upungufu wa vyumba vya madarasa pamoja na mabweni.



Mtaalamu wa Tiba Asili, Said Mbogo, akizungumza na waandishi wa habari katika Mtaa wa Miganga, Kata ya Mkonze, mkoani Dodoma aakitoa tahadhari kwa Watanzania kujihadhari na wimbi la matapeli wa tiba hiyo, wanaojitokeza na kudai kuwa wana dawa ya mimea ya asili inayoweza kutibu Covid-19. Kushoto ni Mtafiti na Mganga wa Tiba Asili, Benjamin Mzuri. **PICHA: PETER MKWAVILA.**

# COSTECH yaahidi kuwaendeleza wabunifu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TUME ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) imeahidi kuendelea kuboresha mawazo ya wabunifu, ili waweze kupiga hatua kwa kile wanachofanya na kutambulika kimataifa.

Hayo yalibainishwa juzi na Mkurugenzi wa COSTECH, Dk. Amosi Nungu, wakati akielezea namna Tume hiyo inavyowasaidia wabunifu katika kazi wanazobuni kufanya kwa lengo la kujiongezea kipato.

Dk. Nungu alisema COSTECH, imekuwa ikiwajengea uwelewa vijana wabunifu kutambua nini maana ya ubunifu ambapo wakishajua hulazimika kuyaboresha mawazo yaliyowasilishwa ili yalete matokeo chanya kitaifa na kimataifa kwa wabunifu hao.

“Unakuta wabunifu wamebuni vitu mbalimbali kama ndege na vingine, lakini ni kwa ajili ya hapa nyumbani, inakuja kimataifa inabidi tuliboreshe teknolojia aliyoibuni kwa kumuunganisha na taasisi mbalimbali kulingana na bunifu aliyoifanya,” alisema Dk. Nungu.

Alisema vijana wasiogope kuleta mawazo ya bunifu zao COSTECH kwani wao watawasaidia kuziboresha ili ziweze kutengeneza bunifu ambazo zitashiriki katika maonyesho.

Akitolea mfano kwa vijana ambao wanaubunifu wa ufundi gereji, alisema wao hulazimika kuwajengea kumbi ambazo watatumia kujiendeleza katika kile wanachofanya na baadaye hutoka kwenda kufanya kazi hizo wao wenyewe.

Mkurugenzi wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Maulilio Kipanyula, alisema mashindano ya kitaifa ya ubunifu yaliyopangwa kufanyika mwezi Machi, mwaka huu, yamegawanyika katika makundi saba.

Prof. Kipanyula alisema washindi wa tatu kutoka kila kundi watapata zawadi lengo ikiwa ni kushawishi kutengeneza bunifu zilizo bora ambazo zitatoa ushindani.

“Mashidano ya mwaka huu tumeboresha zawadi kwa washindi, mshindi wa kwanza atapata sh million tano, wakati wapili atazawadiwa Sh. millioni tatu, huku watatu ataondoka na Sh. milioni mbili,” alisema Dk. Kipanyula.

HABARI MBEYA

# Taasisi zinazotoa vibali kwa wawekezaji zaonywa urasimu

**Na Nebart Msokwa,** MbeyA

SERIKALI imezitaka taasisi za umma zinazotoa vibali na kukusanya kodi kwa wawekezaji, kuacha urasimu wakati wa kutoa huduma zao ili kuchochea kasi ya uwekezaji mkoani humo.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alitoa onyo hilo juzi, wakati akizindua kituo kipya cha mafuta kilichojengwa na Kampuni ya Mafuta ya Manyanya katika eneo la Kadege jijini Mbeya.

Alisema kumekuwapo na malalamiko kutoka kwa wawekezaji wanaowekeza mkoani Mbeya, kuhusu urasimu mkubwa unaofanywa na taasisi za umma ambao unawakatisha tamaa kuongeza uwekezaji na kutamani kwenda kuwekeza kwenye mikoa mingine ama nchi zingine.

Alizitaja baadhi ya taasisi zinazolalamikiwa na wawekezaji kwa vitendo vya urasimu ni Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Baraza la Hifadhi Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Wakala wa Usalama Mahali pa Kazi (OSHA) na Halmashauri za Miji na Majiji.

"Nimefika hapa leo kutoa message (ujumbe) kwa taasisi zetu za umma kuacha urasimu kwa wawekezaji, tunahitaji taasisi hizi ziwe marafiki na wawekezaji kwa kuwasaidia kuwekeza au kupanua uwekezaji wao na sio kuwa maadui na kuwakwamisha," alisema Chalamila.

Alisema endapo vitendo vya urasimu kwa wawekezaji vitaendelea mkoa hautafika mbali, na pia serikali itakosa kodi inayostahili kwa vile wawekezaji hao wanaweza kuhamia maeneo mengine au kupunguza uwekezaji wao na hivyo kulipa kiwango kidogo cha kodi serikalini.

Akizungumza kwenye uzinduzi huo wa Kituo cha Mafuta, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Amede Ng'wanidako, alisema kuwa uwapo wa wawekezaji wengi ndani ya halmashauri yake una manufaa makubwa kwa wananchi kwa vile wawekezaji hao wanalipa ushuru na kuongeza pato la halmashauri.

Alisema fedha hizo zinazolipwa na wawekezaji ndizo zinazotumika kuwapelekea wananchi huduma muhimu za kijamii kama ujenzi wa shule na miundombinu mingine inayohitajika kwenye jamii.

Mwakilishi wa Kampuni ya Manyanya, Priscus Mwaya, alisema kampuni hiyo ina jumla ya vituo sita vya mafuta ndani ya Halmashauri ya Jiji la Mbeya ambavyo wameviunganisha na mifumo yote ya tozo za serikali.

Alisema kutokana na uwekezaji huo, pia wametoa ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja kwa wakazi wa Jiji la Mbeya, hivyo kuongeza kipato kuanzia ngazi ya familia hadi serikalini.

Mwaya aliiomba serikali kuendelea kuweka mazingira mazuri kwa wawekezaji ili wazidi kujitanua na kuleta manufaa kwa wakazi wa Jiji la Mbeya na taifa kwa ujumla.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila (wa pili kushoto), akisikiliza maelezo kuhusu shughuli za uwekezaji kutoka kwa mmoja wa wafanyakazi wa Kampuni ya Mafuta ya Manyanya, kabla ya kuzindua moja ya vituo vya kampuni hiyo, jijini humo juzi. **PICHA NA NEBART MSOKWA**

# Jamii yahimizwa umakini wa malezi ya watoto

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAZAZI, walezi na jamii mkoani Mbeya, wametakiwa kuongeza umakini katika malezi ya watoto kuanzia nyumbani hadi shuleni ili kukabiliana na vitendo vya ukatili wa kijinsia, ukiwamo ubakaji na ulawiti.

Rai hiyo ilitolewa jana na Ofisa Ustawi wa Jamii Mkoa wa Mbeya, Haika Temu, wakati akizungumza na Nipashe kuhusu vitendo vya ukatili wa kijinsia mkoani humo ambavyo vinawatesa watoto.

Alisema wazazi na walezi wanachochea vitendo vya ukatili kwa watoto kwa sababu wengi wao wanakuwa na majukumu mengi ya uzalishaji mali na kusahau kufuatilia mienendo ya watoto wao wawapo shuleni na nyumbani.

"Wazazi wengi hususani kinamama mkoani Mbeya wanajishughulisha na ujasiriamali wanasahau kuhusu malezi ya watoto, kunahitajika umakini, ili kuwapusha na ukatili kwani muda ambao wazazi wako kwenye majukumu watu wasio mema hutumia mwanya huo kutimiza azma zao," alisema Temu.

Mkurugenzi wa Shirika la Kiota Women Health and Development Organization (KIWOHEDE), Justa Mwaituka, alisema wamejikita kutoa elimu ya uwezeshaji kwa vijana hususani kupata uelewa wa kudai haki zao zinapokiukwa.

Alisema katika kufanikisha hayo KIWOHEDE wanashirikiana na wadau wengine katika kutetea na kupigania haki za watoto na watoto ili kuhakikisha wanaishi maisha ya furaha na kupata huduma zote muhimu.

"Tunajitahidi kushirikiana na wanahabari kupaza sauti za walengwa kwani wao ni daraja kati ya shirika, wananchi na serikali, sasa hivi vitendo vya ukatili vimekuwa vikiongezeka," alisema.

"Tumeanza kuona matukio ya ukatili kwa kiasi kikubwa kuanzia ngazi ya familia hadi ndani ya jamii, watoto kuchomwa moto, vipigo vya wanawake dhidi ya wenza wao na mbaya zaidi vilivyovingi haviripotiwi kutokana na undugu uliopo," aliongeza Mwaituka.

Alisema katika kukabiliana na vitendo hivyo tunatakiwa tuwe na sauti mpya kupinga na kuchukua hatua za kisheria yanapotokea kuanzia taasisi ya familia hadi kwenye jamii.

Ofisa Utamaduni Mkoa wa Mbeya, George Mbijima, aliwashauri wazazi kufuata misingi na utamaduni unaokubalika kwenye jamii ili kulea watoto kwenye mazingira salama.

Alisema vitendo vya ukatili wa kijinsia dhidi ya watoto vinaweza kukomeshwa endapo kila mtu atatimiza wajibu wake kwa kuhakikisha watoto wanapata malezi bora, elimu na ulinzi kwao.

# Walimu wakuu wapewa jukumu kuongeza ufaulu

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

SERIKALI wilayani Rungwe, imewataka walimu wakuu wa shule za msingi kusimamia sheria na miongozo ya elimu na kuwaelimisha wazazi juu ya umuhimu wa kushiriki kwenye usimamizi wa sekta hiyo na kuongeza ufaulu.

Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Julius Chalya, alitoa agizo hilo juzi, alipokuwa anafungua mafunzo ya siku tatu kwa walimu wakuu wa Shule za Msingi mkoani Mbeya ya udhibiti ubora yaliyoandaliwa na Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM).

Mafunzo hayo yanafanyika katika Chuo cha Uwalimu cha Msasani kilichopo Tukuyu wilayani Rungwe na kushirikisha walimu wakuu wa shule za msingi kutoka katika halmashauri zote za Mkoa wa Mbeya.

Alisema wazazi ni wadau muhimu katika kuimarisha ufaulu endapo watashirikishwa na kupewa elimu ya umuhimu wao kushiriki kwenye uboreshaji wa elimu akidai kuwa baadhi huwa hawashiriki kwa sababu hawana uelewa wa kutosha.

"Sasa ni jukumu lenu walimu kuhakikisha wazazi wanashiriki, wapeni elimu ili washiriki kwenye uboreshaji wa elimu, kuna baadhi hawashiriki kwa sababu hawana uelewa wa kutosha kwamba na wao ni wadau kwenye elimu," alisema Chalya.

Alisema mafunzo yanayotolewa kwa walimu hao ni muhimu sana kwenye uboreshaji wa taaluma katika maeneo yao ya kazi na hivyo akawataka kwenda kuwaelimisha walimu wenzao.

Mratibu wa Mafunzo hayo kutoka ADEM, Erick Ngwega, alisema katika kuhakikisha ubora wa elimu mafunzo hayo ya udhibiti ubora yatakuwa endelevu kwa walimu wakuu na maofisa elimu ngazi ya mikoa na halmashauri.

Aliiomba serikali kuendelea kuwaboreshea walimu maslahi yao na mazingira ya kufanyia kazi ili wawe na moyo wa kufanya kazi na kwamba hiyo ndiyo njia pekee ya kuimarisha elimu.

"Haya mafunzo ndiyo tumeanza, lakini yatakuwa endelevu, tumeanza na walimu wakuu, lakini baadaye yatatolewa na kwa maofisa elimu wa ngazi zote ambao ndio wasimamizi wa elimu," alisema Ngwega.

Hata hivyo baadhi ya walimu waliishukuru ADEM kwa kuwapatia mafunzo hayo wakidai kuwa yatawasaidia kufanya kazi vizuri kwa kuzingatia miongozo ambayo wanakumbushwa kwenye mafunzo.





# Upinzani wamfagilia Dk. Mwinyi siku 100

**Na Rahma Suleimman,**

ZANZIBAR

WENYEVITI wa vyama vya upinzani nchini wamempongeza Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, kwa kutimiza siku 100 kuwapo madarakani kwa mafanikio makubwa ikiwamo kutekeleza ilani ya Uchaguzi ya CCM kuelekea katika uchumi wa bluu na sekta ya uwekezaji.

Mwenyekiti wa Chama cha ADA-TADEA Taifa, Juma Ali Khatib, alisema katika uongozi wa Rais Dk. Mwinyi zipo kila aina ya dalili za kuyafikia mafanikio ya kiuchumi na uwekezaji katika sera ya uchumi wa bluu baada ya serikali kuingia katika makubaliano ya maelewano ya ujenzi wa bandari za mafuta na ujenzi wa chelezo.

Alisema makubaliano yaliyotiwa saini ya ujenzi wa bandari ya mafuta maeneo ya Mangapwani na Bumbwini kwa kiasi kikubwa sasa kutaiwezesha Zanzibar kuwa kitovu cha biashara kwa meli kubwa za kibiashara kutia nanga na kushusha bidhaa ya biashara ya mafuta kuifanya kuwa ya kimataifa zaidi.

Khatib ambaye ni Mwakilishi wa kuteuliwa na Rais, alimpongeza Dk. Mwinyi kwa kurejesha maridhiano ya kisiasa ambayo yapo kikatiba ambayo hivi sasa yameondosha siasa za chuki na uhasama na kuwaunganisha tena wananchi wa Unguja na Pemba kisiasa na kiitikadi katika kujenga nchi yao.

Naye Mwenyekiti wa ADC, Hamad Rashid Mohamed, alisema Rais Mwinyi amerudisha matumaini ya wananchi wa Zanzibar katika kujenga nchi yao kuwa moja na kubadilisha maisha ya wananchi kuwa bora katika sekta mbalimbali.

# Mahakama zatakiwa kasi usikilizaji wa kesi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, alizitaka mahakama kuharakisha na kuongeza kasi ya kusikiliza kesi zinazoikabili jamii kwa ajili ya kutoa hukumu kwa wakati.

Alisema Mahakama ya Kadhi Zanzibar ambazo hujishughulisha na kesi za talaka, ndoa pamoja na matunzo kwa watoto na familia yapo malalamiko mengi ya kesi kuchukua muda mrefu, hivyo kusababisha usumbufu katika jamii.

"Ucheleweshaji wa kesi athari zake ni kubwa ambapo husababidha jamii kupata majonzi na simanzi kubwa na kuyumba kwa familia," alisema.

Dk. Mwinyi alisema hayo juzi katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Sheria Mjini Zanzibar.

Aidha, aliitaka ofisi ya Jaji Mkuu kuwachukulia hatua za kinidhamu majaji na mahakimu wote wazembe wanaochelewesha kesi kwa makusudi.

Alisema ucheweleshaji wa kesi ni uonevu mkubwa ambao haukubaliki katika jamii hivyo ni lazima haki itendeke.

Alisema ili kudhibiti fedha za umma na kuweka nidhamu ya matumizi serikalini ni lazima kuharakisha kuanzishwa kwa Mahakama ya Kupambana na Rushwa na Wahujumu wa Uchumi Zanzibar.

Alizitaka taasisi zinazohusiana na masuala ya sheria ikiwamo Baraza la Wawakilishi kutunga sheria ambazo zitahakikisha Mahakama ya kupambana na rushwa na uhujumu wa uchumi inafanya kazi zake kwa mujibu wa sheria.

Alisema Serikali ya awamu ya nane imeingia madarakani, huku akipambana na watendaji wanaotumia vibaya madaraka waliyopewa na kujishughulisha na vitendo vya wizi na ubadhirifu wa mali ya umma.

Alizitaja hatua zilizochukuliwa tangu aingie madarakani ni kuwasimamisha kazi watendaji waliobainika na matukio ya ubadhirifu wa mali za umma baada ya kupokea ripoti ya tuhuma hizo kutoka kwa mamlaka ya kupambana na rushwa na uhujumu wa uchumi Zanzibar (ZAECA).

"Kipaumbele cha serikali ni kupambana na watendaji wanaojishughulisha na ubadhirifu wa mali za umma, tunataka kuweka nidhamu ya matumizi ya fedha za serikali," alisema.

Naye Jaji Mkuu wa Zanzibar, Omar Othman Makungu, alizitaka taasisi zinazoshughulikia mwenendo wa kesi kuongeza weledi na utaalamu utakaohakikisha unakamilisha matukio hayo kwa wakati na kuanza kusikilizwa kesi mahakamani.

Pia alilitaka Jeshi la Polisi kuacha kuwabambikizia kesi wananchi na zipo kesi nyingi zinazofikishwa mahakamani zinakosa ushahidi wa kutosha na matokeo yake kuachiwa huru watuhumiwa.

Maadhimisho ya Siku ya Sheria yanaashiria kuanza kwa mwaka wa mahakama kutekeleza majukumu yake ikiwamo kusikiliza kesi ambapo mwaka huu Mahakama Kuu ya Zanzibar imejipanga kusikiliza kesi kwa haraka na kutoa hukumu katika kipindi kifupi kwa kuzingatia sheria.



Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), Jaji Hamid Mahmoud (kulia), akitoa maelezo kuhusu uchaguzi mdogo wa wadi ya Kinuni, kwa wadau wa uchaguzi huo, mjini Zanzibar juzi, unaotarajiwa kufanyika Machi 28, mwaka huu. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Waziri akerwa uchafu katika vituo vya utalii

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Utalii na Mambo ya Kale, Lela Mohamed Mussa, amesema haridhishwi na hali ya uchafu uliopo katika vivutio vya utalii ikiwamo fukwe.

Alisema uchafu katika maeneo ya utalii husababisha kupoteza haiba ya Mji wa kitalii wa Zanzibar na kuhatarisha usalama wa afya kwa wageni.

Aliyasema hayo katika uzinduzi wa kampeni ya usafi kwa maendeleo ya utalii katika Kisiwa cha Kwale Mkoa Mjini Magharibi Unguja.

Waziri huyo aliwataka wakuu wa wilaya kuanzisha siku maalum kwa ajili ya kusafisha vivutio vya utalii ikiwamo fukwe na visiwa ambavyo watalii hufika huko kwa shughuli mbalimbali.

Aliwataka wakuu wa wilaya kuweka siku maalum ya kila mwisho wa mwezi kwa ajili ya usafi katika vivutio vya utalii, ili kupambana na taka na uharibifu wa mazingira unaosababisha vivutio hivyo kukosa haiba kwa wageni wanaoingia nchini.

"Uchafu katika maeneo unahatarisha usalama wa afya kwa wageni hasa wale wanaopata huduma ya vyakula njiani inabidi usafi uzingatiwe na kuwekwa mazingira safi," alisema waziri huyo.

Pia waziri huyo aliitaka Halmashauri ya Magharibi B kusimamia na kuhakikisha visiwa vinakuwa safi na kuandaa tunzo maalum ya usafi kwa wafanyabiashara wa utalii.

Aidha, amesema Zanzibar ni moja ya visiwa vichache vilivyofaidika kupitia biashara ya utalii, ambao ni sekta mama inayochangia uchumi wa nchi kwa asilimia 30.

Hata hivyo, Waziri Lela alipongeza jumuiya kwa kuwawezesha vijana katika kujiajiri na kuajiriwa (Zanzibar Empowerment Organization) pamoja na wawekezaji katika sekta ya utalii kwa kufanikisha kampeni ya usafi katika vivutio vya utalii ambayo itakuwa endelevu nchi nzima kwa kuendeleza na kuunga mkono jitihada za uchumi wa bluu.

Naye Katibu wa Zanzibar Empowerment Organization, Fatma Sarahani, amempongeza Waziri wa Utalii kwa kuwaunga mkono kukubali kuzindua mradi huo ambao utawasaidia vijana kutatua changamoto za ajira pamoja na kuviweka safi vivutio vya utalii.

Alisema kwa kutumia fursa zilizopo wamebuni miradi maalum na kuandaa mikakati ya muda mrefu na mfupi kwa lengo la kuwatafutia ajira katika maeneo yao wanayoishi ili kufaidika na sekta ya utalii.

Katika shughuli hiyo ya usafi wa kisiwa cha Kwale, Waziri Lela, alimteua msanii wa kizazi kipya Zuhura Othamn Soud (Zuchu) kuwa Balozi wa utalii Zanzibar.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


**NAFASI ZA KAZI**

ualimu diploma science,hesabu na kiingeereza 0783298900

***Uza,***
***Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa***


## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ANDREW IDDI MAKASI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 921 DES TOYOTA PORTE.** Chassis No. **NNP110014177.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/MAG/RB/75910/2021.**

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika Mahakama ya mwanzo
Mjini Morogoro
Usimamizi wa mirathi
36/2021

Ombi la **SHOMARI SELEMAN MWINYIMVUA** kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **SELEMANI MWINYIMVUA MWANGA**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo **Tarehe 4/3/ 2021** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.
**Tarehe 4/01/2021**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KWITWA SHAURINI MDAIWA**
**(SUMMONS)**
**(MCA/63)**

Mahakama ya Mwanzo -ARUSHA,
Wilaya ya ARUSHA,
Madai Nambari 20/2021
MDAI: **Kibo Trading & Services Ltd-Arusha (ROWLAND KILEO)**
**Dhidi ya**
MDAIWA: **Sadick Traders Co. Ltd,Tengeru-Arusha**
Kwa kuwa Mdai/ Wadaiwa ameleta/wameleta madai yake/yao ya (eleza aina ya Madai hapa chini)
Fika bila kukosa tarehe iliyopangwa kujibu madai ya fedha Tsh. 11,275,000/=
Kwahiyo unahitajiwa/mnahitajiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya tarehe 15-2-2021 asubuhi/alasiri kwa kujibu madai hayo. Fika na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya utetezi wako kama upo. Angalia kama hukuhudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu endapo Mahakama itathibitisha umepokea/ mmepokea kwitwa shaurini, hii, itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/ mmeshindwa
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 4-2-2021

…………………………………………
akimu/ Hakimu Mkazi/ Mahakama ya Mwanzo

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(SUMMONS)**
**(MCA/63)**

Mahakama ya Mwanzo-ARUSHA,
Wilaya ya ARUSHA,
MADAI NAMBARI 17/2021
MDAI: **Kibo Trading & Services Ltd,Arusha**
**Dhidi ya**
MDAIWA: **Afrael Nnko**
Kwa kuwa Mdai/ Mdaiwa ameleta/ wameleta madai yake/ yao kwamba (Eleza hapa habari za Madai)
Fika mahakamani kujibu madai ya fedha TSHS 5,170,000/=
Kwahiyo unahitajiwa/mnahitajiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya tarehe 15-2-2021 asubuhi/alasiri kwa kujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo,ni lazima kuleta Mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo. Angalia kama hukuhudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu,mahakama ikithibitisha kama umepokea/mmepokea kwitwa shaurini hii, itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/ mmeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 4-2-2021

……………………………………………..
Hakimu/ Hakimu Mkazi/ Mahakama ya Mwanzo

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA JIJI MBEYA**

Unapojibu tafadhali taja
Kumb na.3351/15/azt
19 Juni 2020
Kwa yoyote anayehusika

**SHERIA YA USAJILI WA ARDHI (SURA 334)**
**KUPOTEA KWA BARUA YA TOLEO PAMOJA NA STAKABADHI ZA MALIPO YA KIWANJA**

Barua ya toleo (letter of offer) ya kiwanja pamoja na stakabadhi za malipi ya kiwanja (new offer charges & land rent receipts) . kiwanja na. 25 kitalu 42 majengo, jiji la mbeya
Mmiliki aliyeandikishwa : **JACOB KABISA wa S.L.P 146 MBEYA**
Muombaji: **FROLA SIMON NKWAMA wa s.l.p 149 MBEYA**
Ardhi: **kiwanja na 17 kitalu 29 sokomatola , jiji la Mbeya**

TAARIFA IMETOLEWA kwamba barua ya tolea (letter of offer) ya kiwanja pamoja na stakabadhi za malipo ya kodi ya kiwanja ya kumiliki ardhi (new Offer Charges & Land Rent Receipts) vilivyotajwa hapo juu vimepotea na ninakusudia kutoa nakala halisi ya barua ya tolea (letter of offer) ya kiwanja pamoja na stakabadhi zote za malipo ya kodi ya kiwanja badala yake iwapo hakuna kipingamizi chochote kitakachojitokeza ndani ya muda ya mwezi mmoja tokea tarehe ya taarifa hii.
Barua ya toleo (letter of offer) ya kiwanja pamoja na stakabadhi za malipo ya kodi ya kiwanja (new offer) and land rent receipts) halisi vikionekana virudishwe halmashauri ya jijhi la mbeya S.L.P 149 mbeya

**Imetolewa na**
**Afisa mtuule**
**Halmashauri ya jiji la mbeya**

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**ELICA DANIEL MHALILA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T.176 APD CHASSIS NAMBA FK417E720720.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.
**TAARIFA YA POLISI MBE/MBE/RB/587904/2021**

---

**GSP AUCTION MART**

## TAARIFA KWA UMMA

Tangazo lililotoka tarehe 9/2/2021 kwenye gazeti la Nipashe kulikuwa na makosa ya tarehe iliyokuwa inasomeka tarehe 19/2/2020. Usahihi wake isomeke tarehe 19/2/2021. Tunaomba radhi kwa usumbufu uliojitokeza. Taarifa zingine zinabaki kama zilivyo.

**GSP AUCTION MART**
**+255 654 922 892,**
**+255 687 638 679.**

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**ABDULWAHID MOHAMMED** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 129 BLH** AINA YA **TOYOTA MARK II.** KWA YEYOTE ATAKAYE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI TAARIFA YA POLISI **KAH/TR/RB/47/2021**

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**CATHOLIC DIOCESE OF KAHAMA** Wanatangaza kupotelewa na kadi ya Gari aina ya **HILUX** yenye namba za usajili **T.410 AMU.** Yenye Chassis no. **LN850140240** na Engine no. **2L3734015.** Yoyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo jirani yake. Taarifa ya Polisi. **KAH/TR/RB/55/2021.**

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya mwanzo**
**Mjini Morogoro**
**Usimamizi wa mirathi**
**32/2021**

Ombi la **NASSIR HASSAN CHUMA** kuteuliwa **ABDUL CHUMA KILAMA** msimamizi wa mirathi marehemu **HASSAN CHUMA KILAMA**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo **Tarehe 15/2/ 2021** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo .
Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.
**Tarehe 8/02/2021**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo**
**Wilaya ya Moshi Mjini**

Kituo cha Moshi Mkoa Kilimanjaro
Shauri la Madai/Ndoa Na 32 2021
Jina la Mdai Valency R. Kwayi
Jina la Mdaiwa Ester E. Kibanga

**KUITWA SHAURINI SHAHIDI KATIKA SHAURI LA MADAI**
(Kanuni ya 31 ya Kanuni za Utaratibu wa Madai katika Mahakama za Mwanzo)

Kwa **ESTER E. KIBANGA**
Anuani **MOSHI MJINI /BOMA HAI**
Makazi **BOMANGOMBE HAI**
Simu **0717228750**

**Barua Pepe………………………………**
UNAAMRIWA kuhudhuria mbele ya Mahakama hii tarehe 16 Mwezi February Mwaka 2021 saa 3:00am asubuhi/mchana ukiwa ni shahidi katika shauri lililotajwa hapo juu bila kukosa
Kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikiliza shauri , unatakiwa kuleta vielelezo muhimu vinavyohusu shauri hili
Endapo hautohudhuria katika siku hiyo iliyopangwa , hati ya kukamatwa dhidi yako itatolewa.
Hati hii imetolewa kwa amri na muhuri wa Mahakama leo tarehe 5 Mwezi February , 2021
HAKIMU
Imepokelewa Leo Tarehe ……Mwezi……Mwaka………………… ( Sahihi ya Shahidi)
Nmewasilisha Wito wa kuitwa shaurini kwa shahidi leo tarehe ….Mwezi …..Mwaka
(Sahihi ya Mwasilisha Wito wa Kuitwa Shaurini)

---


**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII



**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Mume jela miaka 30 kisa kumkata mkewe mikono

**Nairobi, KENYA**

MAHAKAMA mjini Machakos, imepitisha hukumu ya kifungo cha miaka 30 gerezani kwa Stephen Ngila Thenge, baada ya kupatikana na hatia kwa kosa la kumkata mkewe mikono, mwaka 2016.

Mikono miwili ya Jackline Mwende ilishambuliwa vibaya na mume wake na kukatwa kwa kutumia kisu kikubwa, sababu alishindwa kumzalia watoto.

Tukio hilo linatajwa kutokana na ugomvi uliotokea nyumbani.

Kisa hicho kilitokea Kijiji cha Kathama, eneo la Masii katika kaunti ya Machakos, licha ya wawili hao kuwa kwenye ndoa kwa miaka saba.

Mikono ya Jackline ilikatwa na mumewe kuanzia kwenye kifundo Julai 24, mwaka 2016.

Kando na kukatwa mikono, Jackline pia alipata majeraha mabaya kichwani na mgongoni.

Ndugu zake walisema kuwa wanandoa hao walikuwa na matatizo na kwamba Jackline alitaka kumwacha mumewe, ingawa alishauriwa kutofanya hivyo na kiongozi wa dini.

"Sijui kwa nini alikuwa akinilaumu licha ya sisi sote kwenda hospitalini mwaka uliopita na kwamba daktari alisema kuwa ni yeye aliyekuwa na tatizo la kuzaa, ambalo linaweza kurekebishwa," alisema Jackline.

Wakati huo, katika mahojiano na gazeti na Daily Nation, Jackline alisema kuwa hali hiyo ilichangia aanze uhusiano mwingine na ikaripotiwa kuwa ni mjamzito.

Jackline alisema, alikuwa na haja ya kuwa na watoto ndipo akaanza uhusiano na mwanaume mwingine, ili kuokoa ndoa yake, ijapokuwa mumewe hivi sasa aliyefungwa jela, kagundua.

"Nilikuwa ninataka mtoto. Nilikuwa na haja ya mtoto na pia ibilisi alisababisha mimi kutembea nje ya ndoa yangu.

Haikuwa vizuri kufanya hivyo, ninajua watu watanihukumu vikali kwa sababu ya hilo. Kwa vile niko hai na nitajifungua mtoto hivi karibuni, nina matumaini licha ya kupitia taabu," alisema Jackline.

***BBC***




Mwanamke mmoja inadaiwa alijeruhiwa kichwani wakati wa maandamano, Polisi wakilazimika kutumia risasi za mpira na maji ya kuwasha kudhibiti maelfu ya waandamanaji ikiwa ni siku ya tatu ya maandamano, mjini Nay Pyi Taw, nchini Myanmar. **PICHA/REUTERS**

# Viongozi wa waasi ndani ya baraza jipya mawaziri

**Khartoum, SUDAN**

WAZIRI Mkuu wa Sudan, Abdalla Hamdok, ametangaza baraza jipya la mawaziri likihusisha viongozi wa zamani wa waasi ambao walikuwa sehemu ya mkataba wa Amani uliosainiwa mwezi, Oktoba.

Hamdok alivunja baraza lililopita siku ya Jumapili kwa ajili ya kuunda serikali ya umoja.

Mawaziri wawili walichaguliwa kutoka kwenye jeshi, ikiwamo kutoka kwenye vikosi vya uhuru na mabadiliko, vilivyoongoza maandamano yaliyomwondoa Omar al-Bashir, madarakani.

Waziri Mkuu pia alimteua kiongozi wa zamani wa waasi na mwana uchumi, Gibril Ibrahim kuwa Waziri wa Fedha.

Hatua hiyo inakuja wakati nchini humo kuna upungufu wa chakula na mafuta kupanda pia kukiwapo mfumuko wa bei.

Bado kuna wanajeshi katika Baraza la Mawaziri la Hamdok, ambalo ni ukumbusho wa ndoa ngumu kati ya wanajeshi na raia, wakati Sudan ikiwa kwenye kipindi cha mpito kuelekea demokrasia.

Hamdok anadaiwa kuteuwa mawaziri wenye utaalamu suala ambalo linasemekana kuwakasirisha wanajeshi.

Tangu Julai mwaka jana, nafasi saba za uwaziri zimekuwa zikishikiliwa na makaimu, ikiwamo wizara ya fedha.

Baraza jipya lenye mawaziri wengi ni kufuatia mkataba wa Oktoba kati ya serikali na baadhi ya makundi ya uasi.

Mkataba huo ulifanywa kwa lengo la kumaliza ghasia kwenye eneo la Darfur na Kusini mwa Sudan.

***VOA***

## Jaji Mkuu adaiwa kuhusika njama kumpindua rais

**Port-au-Prince, HAITI**

WATU 20 akiwamo Jaji wa Mahakama Kuu na Mkuu wa Polisi, wamewekwa kizuizini kwa madai ya kupanga njama ya jaribio la kufanya mapinduzi kumuua rais.

Watu hao inadaiwa kupanga njama ya kutaka kumuua Rais Jovenel Moise wa Haiti na kuipindua serikali yake.

Rais Moise, alizungumza na waandishi wa habari katika Uwanja wa Ndege wa Port-au-Prince kabla ya kuhamia mji wa Jamcel, akisema kwamba kuna jaribio la kutishia maisha yake.

Alisema njama hizo zilipangwa tangu Novemba, mwaka jana.

Rais, Moise alibainisha kuwa ana taarifa watu 20 kuzuiliwa kuhusu tukio hilo, huku akikataa kutoa taarifa zaidi.

Chama cha Mawakili cha Port-au-Prince Young Lawyers, kiliripoti kwamba Jaji wa Mahakama Kuu, Irvikel Dabresil na Mkuu wa Polisi, Antoinette Gauthier walikuwa miongoni mwa waliowekwa kizuizini.

Shirika lililaumu serikali ya Moise kwa kujaribu kukandamiza upinzani kwa kutumia vitisho.

Wakili Reynold Georges pia alizungumza kwa niaba ya upinzani kuhusu kuzuiliwa kwa Jaji Dabresil na kusema: Tunataka aachiliwe mara moja. Mahakama inapaswa kususiwa hadi atakapotolewa.

Katika nchi ya Haiti, Rais Moise alishikilia madaraka kwa muda wa mwaka mmoja kutokana na utata wa uchaguzi wa urais mnamo 2016 na kuanza rasmi urais mnamo Februari, mwaka 2017.

Kwa sababu hiyo, Moise alidai kuwa muhula wake wa urais wa miaka mitano utamalizika Februari, mwaka 2022, wakati vyama vya upinzani vikisema kwamba anapaswa kuacha wadhifa huo mwezi huu.

Maandamano yamekuwa yakifanyika nchini humo tangu Oktoba, mwaka jana na kumtaka Moise aondoke madarakani.

***TRT***

## Bobi Wine atoa ushahidi zaidi kumpinga Museveni

**Kampala, UGANDA**

MAWAKILI wa mwanasiasa wa upinzani nchini Uganda Robert Kyagulanyi, maarufu Bobi Wine, wamewasilisha ushahidi zaidi katika mahakama ya juu, dhidi ya matokeo ya uchaguzi uliomrejesha tena madarakani Rais Yoweri Museveni.

Jopo la majaji likiongozwa na Jaji Mkuu, Alfonce Owiny Doro, linasikiliza ombi hilo katika mahakama hiyo.

Hatuo hiyo, ni baada ya mawakili wa upande wa Bobi Wine kuiomba mahakama iongeze ushahidi zaidi kupinga matokeo ya uchaguzi, uliofanyika mwezi Januari, mwaka huu.

Rais Museveni alipata ushindi wa asilimia 58.08 huku Robert Kyagulanyi akipata asilimia zaidi ya 35, matokeo yanayopingwa vikali na Wine.

Upande wa mawakili wa Rais Museveni, umeshapokea nakala ya mashtaka na siku ya Alhamisi wiki hii wanatarajia kufika katika mahakama ya juu, kupanga siku ya kusikilizwa kwa kesi hiyo, katika kipindi cha siku 45 kulingana na sheria ya uchaguzi nchini humo.

***BBC***



# PSG, MAN CITY BADO WAKOMAA NA MESSI

**MANCHESTER, England**

KLABU za Manchester City na Paris Saint-Germain bado zinamkodolea jicho nyota wa Barcelona, Lionel Messi.


Mkataba wa sasa wa Messi unamalizika mwishoni mwa msimu huu na miamba wa soka wa LaLiga, Barcelona bado hawajafikia makubaliano yoyote na nyota huyo wa kimataifa wa Argentina.

Na klabu hizo mbili kwa pamoja zimekuwa zikihaha kwa muda mrefu kutaka kumsajili mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or.

Paris Saint-Germain ipo kwenye nafasi nzuri zaidi ya kumshawishi nahodha huyo wa Barcelona, Messi kutua kwao, kwa mujibu wa France Football.

Miamba hao wa Ligue 1 wamekuwa wakimkasirisha mara kwa mara kocha wa Barca, Ronald Koeman wanapozungumzia uhamisho wa Messi ambao bado haujajadiliwa.

ESPN imeripoti kwamba, Man City pia inamfuatilia kwa karibu sana Messi, lakini wanasubiri hadi Machi au Aprili kujua kama wataweza kumpata nyota huyo mwenye umri wa miaka 33.




## IBRAHIMOVIC KUONGEZEWA MKATABA AC MILAN

**MILAN, Italia**

MKURUGENZI wa Ufundi wa AC Milan, Paolo Maldini, amebainisha kwamba, Zlatan Ibrahimovic yupo kwenye nafasi nzuri ya kuongeza mkataba na vinara hao wa Serie A.

Ibrahimovic amekuwa kama amefufuka upya tangu alipotua hapo Milan kwa mara ya pili Januari mwaka jana, na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 39 amekuwa kwenye kiwango cha kuvutia mno.

Nyota huyo wiki hii alifikisha mabao 500 aliyofunga ngazi ya klabu wakati Milan ikiibuka na ushindi wa 4-0 kwenye Serie A dhidi ya Crotone.

Wakati mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu, Maldini aliulizwa kuhusu majaliwa ya Ibrahimovic huku Milan pia wakipigania kuwapa mikataba mipya nyota wao, Gianluigi Donnarumma na Hakan Calhanoglu.

"Sisi ni moja ya timu yenye vijana wengi zaidi Ulaya na tunahitaji kiongozi kama Ibrahimovic," alisema Maldini akiiambia BeIN Sports.

"Tulijaribu kumsajili mwaka 2018 wakati alipokuwa anacheza LA Galaxy.

"Alituambia kuongeza mkataba kunategemea na mwili wake, lakini kama ataendelea katika kiwango kama hiki, sioni sababu kwa nini tusimwongeze mkataba.

"Tuna wachezaji watatu ambao mikataba yao inamalizika mwaka 2022, tunaifanyia kazi, lazima pande zote mbili ziwe na furaha, wachezaji ni watu ambao wanafikiria kuhusu dimbani, tuna matumaini tutafikia makubaliano haraka inavyowezekana."

# POGBA AIPA PIGO UNITED

**MANCHESTER, England**

PAUL Pogba atakosa "wiki chache" kwa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer amethibitisha.

Kiungo huyo mshindi wa Kombe la Dunia, Pogba aliirudi kwenye kikosi cha kwanza cha United wikendi iliyopita wakati wakitoka sare ya mabao 3-3 na Everton, lakini alicheza kwa dakika 39.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, alionekana kuumia nyama za paja na alionekana wazi kwamba hangecheza mchezo wa jana Jumanne wa Kombe la FA raundi ya tano dhidi ya West Ham.

Na Solskjaer amethibitisha kwamba, Pogba atakuwa nje ya dimba kwa muda wa wiki chache kutokana na majeraha hayo na atazikosa mechi kubwa.

United itacheza na Real Sociedad nyumbani na ugenini kwenye michuano ya Ligi ya Europa mwezi huu, kabla ya kuwavaa Chelsea kwenye Ligi Kuu mwishoni mwa mwezi na kucheza na Manchester City, Machi 6, mwaka huu.

"Ni majeruhi ambayo yatamfanya kuwa nje ya dimba kwa wiki chache," alisema Solskjaer akiiambia MUTV.

"Ndio kwanza ameanza kupona, yupo chini ya uangalizi wa timu ya madaktari na ninaamini atarudi uwanjani haraka akiwa salama zaidi.

"Bila shaka Paul amekuwa mchezaji muhimu sana kwetu na tutaangalia namna ya yeye kurudi uwanjani haraka, bila kuhatarisha afya yake."

HABARI MICHEZO



# ZIDANE: SIWEZI KUITENGA MADRID

**MADRID, Hispania**

ZINEDINE Zidane amekanusha madai kwamba, anakaribia kuondoka Real Madrid, ingawa hakutoa uhakika wowote juu ya majaliwa yake klabuni hapo huku akieleza kamwe hawezi kuitelekeza klabu hiyo kwa sababu hapo siku zote ni nyumbani kwake.

Bosi huyo wa Madrid, Zidane alibainisha kabla ya mchezo wa Jumamosi dhidi ya Huesca kuwa hatarusha taulo baada ya timu yake kuifunga Deportivo Alaves na kufungwa nyumbani na Levante wakati yeye bado akiwa karantini kutokana na kupata virusi vya corona.

'Los Blancos' hao walipoteza kwenye nusu fainali ya Supercopa de Espana kwa Athletic Bilbao na pia wakatolewa kwenye Kombe la Mfalme (Copa del Rey) na Alcoyano.

Ingawa Madrid walirudi na kuifunga Huesca 2-1 wakipata ushindi wa pili katika mechi sita, Zidane bado anakabiliwa na maswali kuhusu hatima yake.

Wakati alipoulizwa kuhusu majaliwa yake na kwamba ataondoka klabuni hapo, Zidane aliwaambia waandishi wa habari jana, Jumatatu: "Hapana, sikilizeni, jambo la msingi ni kufanya kazi kila siku, hivyo ndivyo tunavyofanya. Kitakachotokea siku nyingine hakihusu leo.

"Kila mmoja hapa, anajaribu kufanya kazi kwa bidii. Hivyo nipo hapa na timu kwa ajili ya timu na si vinginevyo.

"Kila mmoja anaweza kusema lolote, lakini kwa sasa nipo hapa Real Madrid, suala la mimi kuondoka halipo. Na siwezi kusema kwamba, nina uhakika wa kuwa hapa wakati wote, hapana, tufanye yaliyopo mbele yetu kwa sasa."

# Aston Villa kumfunga mazima Grealish

**LONDON, England**

ASNTON Villa wanaripotiwa kuwa wanajiandaa kumpa Jack Grealish mkataba utakaomfanya alipwe pauni 200,000 kwa wiki, ili kumshawishi Mwingereza huyo kubakia klabuni hapo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, alisaini mkataba mpya ambao ulimfanya kulipwa pauni 120,000 kwa wiki msimu uliopita, na ameendelea kuwa katika hali nzuri msimu huu, akifunga mara saba na kusaidia mabao 12 katika michezo 22 kwenye mashindano yote.




Manchester United ilihusishwa sana na mchezaji huyo wa kimataifa wa England msimu uliopita wa kiangazi na bado wanafikiriwa kuwa na hamu ya kumleta staa huyo Old Trafford katika hatua fulani baadaye.

Hata hivyo, kwa mujibu wa mtandao wa 90 min, wamiliki wa Aston Villa wanajiandaa kuwazuia mabingwa hao mara 20 wa England kwa kumpa Grealish mkataba huo mpya mnono.

Tottenham Hotspur, Chelsea na Manchester City hapo awali pia wamehusishwa na mchezaji huyo, ambaye ameweka nyavuni mabao sita na pasi za mwisho 12 kwenye Ligi Kuu England msimu huu.

Aston Villa iliponea chupuchupu kushuka daraja kutokana na kutofanya vizuri msimu wa 2019-20, lakini kwa sasa ni ya nane katika jedwali la Ligi Kuu, ikiwa ni tofauti ya alama tano tu kutoka kwa Liverpool inayoshika nafasi ya nne ikiwa na mchezo mmoja mkononi.

# Shoretire amwaga wino Man United

**MANCHESTER, England**

KINDA wa Manchester United, Shola Shoretire, amesaini mkataba wake wa kwanza kama mchezaji wa kulipwa akiwa na United.

Shoretire amekuwa na wakati mzuri katika kikosi cha wachezaji vijana wa klabu hiyo chini ya umri wa miaka 23 msimu huu akiwa miongoni mwa wachezaji hatari.


Kinda huyo ambaye ni raia wa Nigeria, alikataa kujiunga na klabu kama PSG, Barcelona, Juventus na Bayern Munich ili aendelee kuitumikia United.

Makali ya Shoretire yanaendelea kuchagizwa na ujio wa Amad Diallo ambapo wachezaji hawa wamekuwa na msaada mkubwa kwenye kikosi cha timu hiyo katika michezo miwili waliyocheza pamoja.

Kutokana na kiwango chake, kocha Ole Gunnar Solskjaer ameamua kumjumuisha Shoretire kwenye kikosi cha wachezaji wakubwa na ameanza kufanya nao mazoezi tangu Jumapili.

"Ndoto yangu ya kusaini mkataba wangu wa kwanza na timu ninayoishabikia tangu utotoni imetimia. Ni siku ya kujivunia kwangu na familia yangu.

"Ninawashukuru watu wote kwenye klabu na familia yangu kwa kuniwezesha kufikia wakati huu. Jitihada zinaendelea!" Aliandika Shoretire kupitia ukurasa wake wa Instagram.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# HAZARD: NATAKA KUCHEZA KWA MIAKA MITANO AU SITA

Ndio kwanza nimetimiza miaka 30 kwa jinsi mwili wangu unavyohisi nipo vizuri, matumaini yangu ni...

**MADRID, Hispania**

NYOTA wa Real Madrid, Eden Hazard, amesema anataka kuendelea kucheza kwa angalau miaka mingine mitano au sita, akisisitiza majeraha "si mwisho wa dunia" wakati huu akikabiliwa na tatizo la kuwa fiti pale kwenye dimba la Santiago Bernabeu.

Hazard alisajiliwa kutoka Chelsea kwenda Madrid kwa ada iliyoripotiwa kuwa euro milioni 100 mwaka 2019, lakini muda wake pale kwenye mji mkuu wa Hispania umekuwa ukimbana kutokana na majeraha ya mara kwa mara.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, ambaye atakuwa nje ya dimba kwa wiki "mbili au tatu" kutokana na majeraha ya mguu wa kushoto, ameanza katika mechi 20 tu za LaLiga - sita kati yake zikiwa msimu huu, na amefunga mabao matatu tu.

Hazard ameshindwa kucheza kwa dakika zote 90 katika mchezo wowote wa Madrid msimu huu wa 2020-21 kwenye mashindano yote, lakini mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji bado yupo na mtazamo chanya.

"Nina matumaini ya kucheza soka kwa muda mrefu kadri inavyowezekana, na mara zote najaribu kufurahia mwenyewe uwanjani," alisema akiliambia gazeti la On The Front Foot.

"Linapokuja suala la mwisho wa kipindi changu cha kucheza, naweza kuangalia nyuma kwenye mafanikio yangu, lakini kipaumbele changu ni kucheza vizuri na kuendelea kufurahia soka.

"Sifikirii wapi nitakuwa baada ya miaka michache ijayo, najaribu kufikiria kuhusu mechi inayokuja na mazoezi yanayofuata.

"Ndio kwanza nimetimiza umri wa miaka 30 kwa jinsi mwili wangu unavyohisi nipo vizuri, matumaini yangu naweza kucheza kwa angalau miaka mitano au sita."

"Nina bahati kwamba, ninapoumia natulia nyumbani, nina familia ambayo nakuwa nayo bega kwa bega," aliongeza kusema Hazard.

"Si mwisho wa duniani kwangu mimi kwa sababu naweza kutumia muda na watoto wangu, wakati unapoumia na kuwa mwenyewe unaweza kuwa na wakati mgumu sana kwako, nina bahati kwamba, nina familia ya kunipa sapoti."

## KWA UFUPI

**MAN CITY YAMTAKA MESSI**

MANCHESTER City bado wanataka kumsajili mshambuliaji wa Barcelona, Lionel Messi mwenye umri wa miaka 33, katika dirisha la msimu huu wa kipindi cha majira ya joto, lakini wanajiandaa wakisubiri mpaka Machi au Aprili. ***(ESPN)***

**ZIDANE AGOMA KUJIANIKA REAL**

KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane, amekataa kuthibitisha ikiwa ataendelea kubaki Bernabeu, baada ya mkataba wake kumalizika mwaka 2022. ***(Mirror)***

**CHELSEA YAJITOSA KWA ALABA**

CHELSEA itamchukua David Alaba ambaye mkataba wake ndani ya Bayern Munich unamalizika mwishoni mwa msimu huu - ikiwa tu beki huyo wa kushoto wa Austria mwenye umri wa miaka 28, atapunguza kiwango cha mshahara anachotaka, kiasi cha pauni 400,000 kwa wiki. ***(Telegraph)***

**BECKHAM AMTAKA GIBBS**

INTER Miami inayomilikiwa na David Beckham inafikiria kumnasa mchezaji wa nafasi ya ulinzi wa West Brom, Kieran Gibbs mwenye umri wa miaka 31, kwa uhamisho huru mwishoni mwa msimu huu. ***(Athletic, via Mail)***

**LUKAKU, INGS WAWINDWA CITY**

MSHAMBULIAJI wa Inter Milan, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 27 raia wa Ubelgiji, na Danny Ings, 28, ni miongoni mwa wachezaji wanaotazamwa na Manchester City wakati huu klabu hiyo ikitafuta mshambuliaji mpya. ***(Athletic)***

**KONATE AGOMBEWA ENGLAND**

MANCHESTER United imeweka wazi kuwa inalenga kumsajili, Ibrahima Konate wa RB Leipzig mwenye miaka 21, kama beki muhimu kwao. Hata hivyo, watapata upinzani kutoka kwa Liverpool na Chelsea ambazo nazo zinamwania.***(Independent)***

**SHORETIRE ASAINI MKATABA UTD**

WINGA wa Nigeria, Shola Shoretire mwenye umri wa miaka 17, amesaini mkataba wa kwanza na Manchester United, ingawa pia PSG, Barcelona, Juventus na Bayern Munich zilikuwa zikimtolea macho. ***(Mail)***

**CHRISTENSEN AMKUNA TUCHEL**

KIWANGO alichoonyesha mlinzi wa kati wa Denmark, Adreas Christensen mwenye umri wa miaka 24, pengine ndicho kilichomshawishi kocha wa Chelsea, Thomas Tuchel kutohitaji kumsajili mchezaji wa nafasi ya ulinzi katika dirisha la usajili la msimu ujao wa majira ya joto. ***(Football London)***

**MOYES AONYESHA UBAHILI**

KOCHA wa West Ham, David Moyes, amesema alikataa kutumia pauni milioni 15 hadi 20 kwa mshambuliaji mpya katika dirisha la uhamisho la Januari. Mshambuliaji pekee anayetambuliwa, ni Michail Antonio mwenye umri wa miaka 30, ambaye anapambana na uchovu. ***(Goal)***

**MONREAL KUONGEZA MKATABA**

MLINZI wa zamani wa Arsenal, Nacho Monreal mwenye umri wa miaka 34, yuko kwenye mazungumzo ya kuongeza mkataba ndani ya klablu ya Real Sociedad. Mkataba wake wa sasa unatarajiwa kumalizika Juni mwaka huu. ***(Marca)***

**PSG, MAN CITY VITANI**

MSHAMBULIAJI wa Inter Milan, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 27, ameingia kwenye vita Paris St-Germain na Manchester City zikiwa zinawania saini yake. ***(Sky)***

HABARI MICHEZO

# NAHODHA PRISONS ASTAAFU SOKA RASMI AKIMTAJA OKWI

**Na Adam Fungamwango**

NAHODHA wa Tanzania Prisons, Laurian Mpalile, ametangaza rasmi kustaafu kucheza soka, huku akimtaja mshambuliaji Emmanuel Okwi kuwa ndiye mchezaji aliyekuwa akimnyima usingizi kila wanapoelekea kucheza dhidi ya timu yake.

Mpalile, mwenye uwezo wa kucheza beki wa pembeni na wa kati, amesema Okwi wakati akicheza soka Tanzania alikuwa ni mchezaji msumbufu ambaye beki yeyote huwa hapendi kukutana naye.

"Kama kesho tunakwenda kucheza mechi ambayo Okwi yupo, basi unakuwa unamuwaza tu kesho sijui itakuwaje, unajua sisi mabeki mara nyingi hatupendi sana kukutana na wachezaji mchachari kama yeye," alisema mchezaji huyo.

Aliwataja wachezaji wengine ambao walikuwa wakimpa wakati mgumu akikutana nao dimbani kuwa ni Simon Msuva na Sosteness Manyasi.

Wakati Okwi akiwa mchezaji wa Simba kwa misimu mingi, Msuva alikuwa winga wa Yanga na Manyasi wakati huo alikuwa akiitumikia JKT Ruvu, kwa sasa ikiitwa JKT Tanzania.

Kwa sasa wachezaji hao wote hawachezi Ligi Kuu Tanzania Bara, Manyasi akiwa ni mwajiriwa wa Jeshi la Kujenga Taifa kwa sasa, Okwi akicheza soka la kulipwa nchini Misri Klabu ya Al Ittihad na Msuva anaitumikia Wydad Casablanca ya Morocco.

Katika maisha yake ya soka, Mpalile alisema kuwa ameitumikia klabu hiyo kwa miaka 15, hivyo kwa sasa anastaafu na kwenda kupangiwa majukumu mengine kwenye kikosi cha timu ya vijana.

Mpalile ni mwajiriwa wa Jeshi la Magereza, huku akisema kuwa soka limempatia ajira, nyumba na kuwa na familia. Aliwataja baadhi ya mabeki wenzake ambao anawahusudu kuwa ni Amir Maftah na Juma Jabu ambao kwa sasa hawachezi timu yoyote ya Ligi Kuu, na David Luhende ambaye anaichezea Kagera Sugar.

# Johnnie Walker yapania kukuza gofu nchini

**Na Mwandishi Wetu**

KWA kutambua umuhimu na mchango mkubwa wa mchezo wa gofu kwa maendeleo ya taifa na watu wake, Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL) kupitia kinywaji chake cha Johnnie Walker imejitosa kuwa mdhamini wa mashindano makubwa kabisa ya gofu kwa ukanda wa Afrika Mashariki yanayojulikana kama Johnnie Walker Waitara Trophy.

Hiyo si mara ya kwanza kwa kampuni hiyo kufanya hivyo, kwani historia ya SBL kudhamini mchezo wa gofu inaanzia mwaka 2019, ambapo kwa mara ya kwanza ilidhamini mashindano hayo kupitia Bia yake ya Serengeti Lite kabla ya Johnnie Walker kuingia mwaka 2020.

Johnnie Walker ni kinywaji cha kimataifa chenye chimbuko lake nchini Scotland na wakati kinadhamini mashindano hayo makubwa, kinasherehekea pia miaka 200 tangu kuanza kutengenezwa na kufanya kuwa moja ya kinywaji chenye historia kongwe duniani kama ulivyo mchezo wa gofu ambao ulianzishwa takriban miaka 600 iliyopita.

Wakati mashindano ya Johnnie Walker Waitara Trophy kwa mwaka 2020 yameshafanyika katika viwanja vya Gofu vya Lugalo jijini Dar es Salaam huku yakishuhudiwa zaidi ya wachezaji 180 wakishiriki, baadhi wakiwa wametoka nje ya nchi, SBL imesema huo ni mwanzo tu kwa kuwa malengo yake ni kufanya mambo makubwa zaidi kupitia mchezo huo.

Akizungumza wakati wa hafla ya utoaji zawadi kwa washindi, Mkurugenzi Mtendaji wa SBL, Mark Ocitti, alisema kinywaji cha Johnnie Walker kitaendelea kudhamini mashindano hayo kwa siku zijazo pamoja na kusaidia jitihada mbalimbali zinazolenga kukuza mchezo wa gofu hapa nchini.



Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama nchini, Generali Venance Mabeyo, akizungumza wakati wa halfa ya utoaji zawadi baada ya mashindano ya Gofu ya Johnnie Walker Waitara Trophy kumalizika katika viwanja vya Gofu Lugalo jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **MPIGAPICHA WETU**

Mkurugenzi huyo aliwaambia washiriki wa hafla hiyo ya utoaji zawadi kuwa Johnnie Walker inajivunia kuwa sehemu ya mashindano hayo na kama kinywaji kinachoamini katika kusonga mbele, kitaendelea kusimama bega kwa bega na Klabu ya Gofu Lugalo katika kuendeleza mchezo huo.

Kwa upande wa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama nchini, Generali Venance Mabeyo, aliishukuru SBL na kinywaji cha Johnnie Walker kwa kuwa wadau muhimu katika maendeleo ya michezo hapa nchini ikiwa ni pamoja na mchezo wa gofu.

Mkuu huyo wa majeshi, alisema mashindano hayo yamesaidia kuvumbua vipaji vya wachezaji wachanga ambao watakuwa tegemeo kwa siku zijazo.

"Baadhi ya washindi ni wachezaji vijana ambao wanaweza kuendelea kujiendeleza na kuwa nyota wakubwa duniani na kuitanga nchi yetu kimataifa.

"Kampuni ya SBL imekuwa ni mdau mkubwa kwa maendeleo ya michezo na gofu. Hii ni mara ya pili kwa kampuni hii kudhamini mashindano haya kupitia bidhaa zake mbalimbali ikiwamo bia ya Serengeti Lite na mwaka huu kupitia kinywaji cha Johnnie Walker, napenda kutoa shukrani na pongezi nyingi kwa kujitoa kwao," alisema.

Akizungumza muda mfupi baada ya kupata zawadi ya fedha taslimu shilingi milioni moja kama mshindi wa kwanza kwa wachezaji wa kulipwa, Bryson Nyenza ambaye ni mchezaji kijana kutoa Klabu ya Gofu Lugalo, aliishukuru Johnnie Walker kwa kutoa udhamini wenye tija ambao umemwezesha kuibuka mshindi.

"Udhamini wa Johnnie Walker umewezesha kuwapo kwa maandalizi mazuri, viwanja viliandaliwa vizuri na kila kitu kilikuwa vizuri kabisa," alisema

klabu mbalimbali za gofu zikiwamo, Arusha Gymkhana, Mufindi Club, Morogoro Gymkhana, Dar es Salaam Gymkhana, Sea Cliff Golf Club Zanzibar, Kili Golf pamoja na TPC Golf Club zilishiriki michuano hiyo.

## Azam FC, Coastal ni kisasi na pointi

**Na Saada Akida**

BAADA ya kulazimisha sare ya mabao 2-2 dhidi ya Simba, Kocha Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati, amesema sasa wanahitaji kwenda kulipa kisasi dhidi ya Coastal Union ambayo msimu uliopita iliwafunga nje ndani katika michezo yote miwili ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Vivier alisema wamejipanga vizuri kuhakikisha wanarejea na pointi tatu kutoka Uwanja wa Mkwakwani kesho, Alhamisi kwa kuwa wanafahamu wanapokutana na Coastal Union mechi huwa ngumu.

"Hatuna historia nzuri sana na Uwanja wa Mkwakwani, tunahitaji kupata matokeo chanya ikiwamo pointi tatu, tunahitaji kulipa kisasi, tunatambua wenyeji wetu wamejipanga kuendeleza kile ambacho wamekifanya nyuma," alisema Vivier.

Azam kwa sasa ipo nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara ikiwa na pointi 33 baada ya mechi 18 huku Coastal Union ambayo nayo imecheza idadi hiyo ya mechi ikiwa na alama 20 katika nafasi ya 13.

## ZAHA yageukia vipaji msingi na sekondari

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MSIMAMIZI Mkuu wa Maendeleo ya Vijana wa Chama cha Mpira wa Mikono Zanzibar (ZAHA), Kombo Ali Kombo, amesema kwa sasa wameanzisha mpango wa kufundishwa mchezo huo katika shule za msingi na sekondari visiwani hapa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kombo alisema lengo la mpango huo kupelekea mchezo huo shuleni ili kupata wachezaji vijana wengi tofauti na ilivyo sasa.

Alisema lazima vijana wenye umri mdogo waandaliwe mapema ili kupata wachezaji ambao watautumikia mchezo huo kwa kipindi kirefu.

"Chama tumeona ili kutimiza malengo yetu na yawe endelevu basi ni bora tukaendeleza vijana katika ngazi za nchini kabisa, huku tutapata wachezaji ambao wanahamu ya kucheza mchezo huu," alisema.

Alisema mpango huo kwa sasa unaendelea kisiwani Unguja pekee na kwa baadaye wataupeleka kisiwani Pemba ili kutoa fursa kwa wanafunzi waliopo shuleni kuufahamu vema mpira wa mikono.

Hata hivyo, alisema Chama cha Mpira wa Mikono Zanzibar pia kinaendelea na mpango wake wa kila siku za mapumziko kuzikusanya timu zote za mchezo huo zilizopo Unguja ili kuzipa elimu ya namna bora ya kuzifundisha timu zao na kuziandaa vizuri kuweza kupata wachezaji wenye viwango watakaoweza kutoa ushindani katika mashindano ya kimataifa ambayo wamekuwa wakialikwa.

Michezo
Jumatano Februari 10, 2021
Nipashe



HAZARD: NATAKA KUCHEZA KWA MIAKA MITANO AU SITA HABARI UK 22

# SIMBA SC NA MAJEMBE 27 WAIFUATA VITA KWA VITA

●●●Gomes ataka kila nafasi bao akisisitiza kuanza na ushindi huku uongozi ukisema kila kitu…

**Na Mwandishi Wetu**

MABINGWA wa Ligi Kuu Bara wenye dhamana ya kuipeperusha bendera ya Tanzania kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba, ambao pia wanabeba jukumu hilo kwa nchi za Afrika Mashariki na Kati kutokana na kuwa timu pekee katika mashindano hayo kwenye ukanda huu, wameelekea nchini DR Congo tayari kwa vita dhidi ya AS Vita.

Simba ambayo ipo Kundi A pamoja na AS Vita, Al Ahly ya Misri na Al-Merrikh ya Sudan, imeondoka nchini jana mchana kupitia Ethiopia ikiwa na wachezaji 27 wote wakiwa tayari kwa mchezo huo wa kwanza wa hatua ya makundi utakaopigwa keshokutwa, Ijumaa.

Wachezaji 27 waliondoka na kikosi hicho ni Aishi Manula, Beno Kakolanya, Ally Salim, Shomari Kapombe, Joash Onyango, Pascal Wawa, Ibrahim Ame, Erasto Nyoni, Peter Muduhwa, Kennedy Juma, Gadiel Michael, Mohamed Hussein 'Tshabalala', Taddeo Lwanga na Jonas Mkude.

Wengine ni Rally Bwalya, Said Ndemla, Mzamiru Yassin, Luis Miquissone, Hassan Dilunga, Ibrahim Ajibu, Clatous Chama, Bernard Morrison, Francis Kahata, Meddie Kagere, Miraji Athumani, Chris Mugalu na Junior Lokosa.

Kocha Mkuu wa Simba, Mfaransa Didier Gomes, amesema wachezaji wote aliongozana nao wapo tayari kwa mchezo huo na wana ari kubwa ya kuipambani timu kufanya vizuri katika mechi hiyo ya fungua dimba hatua ya makundi.

Alisema makosa madogo madogo aliyoyabaini kuanzia mechi za kujiandaa na michuano hiyo Simba Super Cup, walipocheza dhidi ya Al Hilal ya Sudan na TP Mazembe ya DR Congo pamoja na michezo miwili ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Dodoma Jiji na Azam FC, tayari wameyafanyia kazi.

"Tunakwenda DR Congo tukiwa na malengo. Tukipata nafasi ya kufunga, tufunge na nimesisitiza hilo, tunaenda tukiwa na kikosi kamili, katika mechi tulizocheza hususan dhidi ya Azam tulishindwa kutumia nafasi lakini tumerekebisha makosa hayo," alisema Gomes.

Gomes alisema haitakuwa mechi rahisi kwa kuwa kila timu inataka kushinda mechi ya kwanza, lakini wanakwenda kupambana na morali wa wachezaji wake katika kufanya vizuri ipo.

Kwa upande wa Ofisa Habari wa Simba, Haji Manara, alisema tayari Simba ilishatanguliza watu wao tangu juzi kwa ajili ya kuandaa mazingira kabla ya timu hiyo kutua na kwa mujibu wa taarifa zilizowafikia kila kitu kimekwenda vizuri ikiwa ni pamoja na hoteli nzuri na uwanja wa mazoezi.

"Tumeshafanya maandalizi yote na hata hoteli tunayoshukia pamoja na uwanja wa mazoezi tumeshaujua, wachezaji wote ambao wanaondoka wapo fiti ni jukumu tu la kocha kuchagua nani aanze, ninaimani kubwa tutashinda," alisema Manara.

Timu hizo pia zilikutana kwenye michuano hiyo hatua ya makundi msimu wa 2018/19 na katika mechi ya kwanza nchini DR Congo, AS Vita ilishinda 5-0 kabla ya kurudiana Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam na Simba kushinda 2-1 hivyo kutinga robo fainali katika kundi lao pamoja na Al Ahly.

Baada ya mchezo huo, katika michuano hiyo ya CAF, Simba itaikaribisha Al Ahly katika Uwanja wa Benjamin Mkapa Februari 23 kisha kati ya Machi 5-6 itakuwa ugenini nchini Sudan kuvaana na Al Merrikh.

## SOMA HIYOOO...




Mshambuliaji wa Bayern Munich, Robert Lewandowski, akishangilia na mchezaji mwenzake moja kati ya mabao mawili aliyofunga wakati wakishinda 2-0 dhidi ya mabingwa Afrika, Al Ahly, katika mechi ya nusu Fainali ya Klabu Bingwa Dunia iliyopigwa Uwanja wa Ahmed bin Ali jijini Al Rayyan, Qatar juzi. Bayern sasa itamenyana na bingwa wa Amerika Kaskazini, Tigres UANL ya Mexico katika mechi ya fainali itakayopigwa kesho, Alhamisi kwenye Uwanja wa Education City jijini Al Rayyan. **PICHA: MTANDAO**

## SIMBA, YANGA KAZI IPO ZIKIVUKA FA CUP

**Na Saada Akida**

DROO ya Raundi ya Nne ya Kombe la Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), maarufu FA Cup, imefanyika jijini Dar es Salaam jana, ambapo mabingwa watetezi, Simba watamenyana na African Lyon huku watani zao, Yanga wakipangwa kumenyana na Kengold FC ya Daraja la Kwanza kutoka Mbeya.

Endapo Simba itashinda mchezo wake huo, itakutana na mshindi kati ya Kagera Sugar au Eagle Stars wakati Yanga kama ikishinda itakutana na mshindi kati ya Sahare All Stars au Tanzania Prisons.

Azam FC watamenyana na Mbuni FC ya Daraja Pili kutoka Arusha, Mtibwa Sugar vs JKT Tanzania, Namungo FC vs Mbeya City, Mwadui FC vs Gwambina FC, Coastal Union vs Ihefu FC, Arusha FC vs Mashujaa FC na Rhino Rangers vs Tunduru Korosho.

Mechi zingine zitaikutanisha Kagera Sugar vs Eagle Stars, Mbao FC vs Ruvu Shooting, Polisi Tanzania vs Kwamndolwa, Dodoma FC vs Kipigwe FC, KMC vs Kurugenzi FC, Sahara All Stars vs Tanzania Prisons na Biashara United vs Transit Camp.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Mashindano wa TFF, Baraka Kizinguto, fainali ya michuano hiyo, itapigwa katika Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani Kigoma huku mechi za nusu fainali zikipigwa katika viwanja viwili tofauti, Uwanja wa Ally Hassan Mwinyi mkoani Tabora na wa Majimaji, Songea.

Alisema tayari mikoa hiyo imeanza kuboresha viwanja vyao kwa kuweka mazingira mazuri ya kucheza nusu fainali hizo mbili pamoja na fainali.

"Hiyo mikoa mitatu ilikuja kuomba kwa ajili ya kuandaa mashindano hayo kwa hatua hizo na imekubaliwa na kupewa vigezo vya kuboresha mazingira ya viwanja, ili kuwa rafiki kwa nusu fainali na fainali," alisema Kizunguto.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042